Kikao cha Kumi na Nane – Tarehe 10 Juni, 2014

(Kikao Kilianza saa 3:00 za asubuhi)

Dua

Mhe. Naibu Spika,(Mhe. Ali Abdalla Ali) Alisoma Dua

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 48

Sheria ya Kudhibiti Ndege Chakavu

Mhe. Jaku Hashim Ayoub (Kny: Mhe. Saleh Nassor Juma) – Aliuliza:-

Kwa kuwa hivi karibuni ndege inayomilikiwa na Kampuni ya ZAN – AIR, ilipata tatizo la kiufundi na hatimae kushindwa kutua salama kwenye uwanja wa ndege wa Pemba na hatimae kulazimika kuingia katika pori jambo lililoleta mshtuko mkubwa kwa abiria pamoja na familia zao. Kwa kuwa hivi karibuni Baraza hili lilitunga Sheria ya Kudhibiti Usajili wa vyombo Chakavu vya Baharini.

Je, ni lini Serikali katika kuhakikisha usalama wa raia na mali zao, wataleta sheria hapa kuzuia matumizi ya ndege chakavu katika anga ya Zanzibar.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano – Alijibu:-

Nakushukuru Mhe. Naibu Spika, kwanza kama ilivyo kawaida tumeamka asubuhi, tunamshukuru Allah kwa kutujaalia uhai, uzima na taufiki ya kufika katika Baraza hili tukufu.

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba sasa nimjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 48 kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, wizara inakubaliana na maelezo ya Mhe. Mwakilishi, kwamba mnamo tarehe 24/01/2014 majira ya saa 07:45 ndege inayomilikiwa na Kampuni ya ndege ya ZAN AIR ilipata tatizo la kushindwa kutua salama katika uwanja wa ndege wa Pemba, na kulazimika kuingia katika pori. Uchunguzi wa tukio hilo bado unaendelea kufanyika ili kubaini chanzo chake na kupendekeza hatua muafaka za kuzuia matukio ya ajali kama hiyo yasiendelee kutokea.

Mhe. Naibu Spika, hata hivyo, sehemu ya suala lake kuhusu ndege chakavu ni kama ifuatavyo. Naomba ieleweke kuwa kikawaida ndege huwa haichakai ikiwa itafuata masharti yaliowekwa na mtengenezaji wa ndege ile yaani aircraft flight manual au cheti kinachoruhusu ndege kuruka certifícate of airworthiness kinachotolewa na Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania (TCAA) ambayo ndiyo yenye jukumu la usimamizi wa usafiri wa anga ikihusisha kazi za ukaguzi na utoaji wa cheti kinachoruhusu ndege kuruka.

Mhe. Naibu Spika, kikawaida ndege yoyote iliyosajiliwa katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa shughuli za kibiashara, kabla haijaruhusiwa kuruka hukaguliwa na Mamlaka husika na kupewa cheti kinachoruhusu ndege husika kuruka, cheti hicho kinaitwa certifícate of airworthiness baada ya kufikia kiwango kinachokubalika kwa kutumia kanuni za ukaguzi wa ndege yaani Airworthiness regulations na masharti ya mtengenezaji wa ndege hiyo aircraft flight manual.

Vile vile, kwa kuzingatia masharti ya watengenezaji wa ndege pamoja na kanuni za ukaguzi wa ndege, ndege yoyote ile hutakiwa kufanyiwa matengenezo makubwa ya engine yaani overhaul baada ya kufikia umri wa miaka 15, ikiwemo kubadilisha engineer hizo na kuweka nyengine mpya, ili kuirejesha katika hali yake ya kawaida na kuendelea kutumika. Utaratibu huu ndio unaotumika duniani kote na kukubaliwa na Jumuiya za Kimataifa zinazosimamia usafiri wa anga duniani na kuridhiwa na nchi yetu.

Kwa maana hiyo, umri wa ndege si kigezo kinachojitegemea cha ubora wa ndege, alimuradi tu itafuata masharti yaliotajwa hapo juu na hivyo kuruhusiwa kuendelea kutumika.

Mhe. Naibu Spika, kulingana na mnasaba huo, wizara haioni sababu kwa sasa ya kutunga sheria ya kuzuia matumizi ya ndege chakavu, kwa vile sheria na taratibu zinazohusiana na matumizi ya ndege zipo na kusimamiwa na taasisi husika, mbayo ni Tanzania Civil Service Authority (TCAA).

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu ya Mhe. Waziri dhamana wa Miundombinu na Mawasiliano, naomba kuuliza maswali mawili madogo tu ya nyongeza. Kwa kuwa ajali hii ni ya pili kutokea katika maeneo ya Zanzibar, tulishuhudia kati ya miezi sita au minane sasa hivi, ndege ya Oman Air na Ethiopian Air Line kugongana katika uwanja wa ndege wa Zanzibar na mpaka hii leo hatujapokea taarifa yoyote.

Kwa majibu yenu ya kawaida Mhe. Waziri serikali iko mbioni, hebu toa hizo mbio zake ni lini tutapata jawabu na uchunguzi haujafanyika hadi hii leo. Kwa kuwa madai ya kwamba utaalamu wa wataalamu ni mdogo wale wanaoegesha ndege pale. Je, ni lini mtawapa utaalamu huo?

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Naibu Spika, swali la pili sikulisikia naomba alirudie.

Mhe. Naibu Spika: Anasema pale wataalamu wenu utaalamu wao ni mdogo, ni lini mtaweza labda kuwapa mafunzo, ili waweze kwenda kimataifa na wao.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Nakushukuru Mhe. Naibu Spika, kwanza ajali iliyotokea aliyoitaja yeye ni tofauti na ile. Ajali ile iliyotokea ya Oman Air na Ethiopian Air Line ni ndege za kimataifa zote mbili, zinaruka katika anga za kimataifa na sio ndege za ndani. Ajali ile ilipotokea hao hao TCAA ndio walioishughulikia na wakawasawazisha. Moja katika jambo lililorekebishwa, kulikuwa na tatizo la kuegesha ndege kwa kutegemea upande. Kwa hivyo, ilirekebishwa kwa kuwa ndege ikae sawa sawa na kiwanja na tatizo hilo limeondolewa kabisa. Ndege zote mbili zilikaa upande katika angle ndio likatokezea tatizo hilo ambalo lilitokezea.

Kwa hivyo, katika mambo ambayo yalipendekezwa na TCAA kurekebishwa ni kwamba ndege kubwa zikija zikae sawa sawa na kiwanja. Kwa hivyo, sasa hivi tatizo hilo limeondoka, kwa sababu ikiondoka ndege haina tatizo la kwenda kugusana na tatizo ndege nyengine.

Suala la pili, kama tulivyosema kwamba kazi ya Mamlaka ya Uwanja wa Ndege ni kuruhusu ndege. kutua na kutumia ile facility zilizopo katika uwanja wa ndege. Lakini utaalamu wa ndege uko kwenye taasisi hiyo inayoitwa TCAA. Kwa hivyo, utaalamu upo na ndio maana ikitokezea ajali wanakuja wao na sisi hatuingilii chochote mpaka wataaalamu hao wa TCAA waweze kutoa kauli yao ndio tatizo hilo liweze kutatuliwa.

Mhe. Jaku Hashima Ayoub: Nilichomuuliza mimi ni lini, kwenye kanuni ya 37 Mhe. Naibu Spika, nilitumia, "waziri au mjumbe yeyote anayeulizwa swali ambalo ana madaraka nalo basi atakuwa na wajibu wa kujibu swali hilo". Nilichomuuliza Mhe. Waziri mimi ni kwamba lini uchunguzi utakamilika ikiwa ni muda mrefu sasa tokea ndege ya Oman Air na ndege ya Ethiopian Air Line, zikiwa ziko chini zimegongana. Nauliza uchunguzi huo ni lini atatuletea Mhe. Waziri?

Mhe. Naibu Spika: Sasa labda nimsaidie, waziri swali mama halikuhusika na ndege ya Oman Air na Ethiopian Air Line, yeye kasaidia tu katika kujibu. Swali lilikuwa ni ndege kutaka kuanguka na alijibu vizuri tu.

Mhe. Jaku Hashima Ayoub: Ni katika kuhakikisha usalama wa raia, katika swali hili lililoulizwa na Mhe. Saleh Nassor Juma. Nazungumzia usalama ndio suala la msingi.

Mhe. Naibu Spika: Sasa tatizo hatujakufahamu unataka nini?

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Aniambie ni lini uchunguzi huo utakamilika na atatuletea lini uchunguzi huo?

Mhe. Naibu Spika: Wa hii ajali ama.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Wa hiyo ajali.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Waziri, mjumbe anataka uchunguzi unaofanywa utamalizika lini kwenye ajali iliyotokezea.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako niseme kwamba Mhe. Jaku Hashim Ayoub hasikilizi. Kwa sababu nimemwambia sisi mamlaka sio wenye kuchunguza, ni TCAA yaani Tanzania Civil Aviation Authority ndio ambao wanachunguza. Kwa hivyo, sio sisi kama mamlaka ni taasisi ambayo wiki iliyopita, mjumbe huyu huyu aliuliza ni wafanyakazi wangapi waliopo katika shughuli za anga. Kwa hivyo, anajua kwamba taasisi hiyo ipo na ni ya Muungano na ndio inayochunguza, mamlaka haiingilii chochote katika uchunguzi wao.

Mhe. Nassor Salim Ali: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi kunipa nafasi ya kuuliza swali moja dogo la nyongeza. Mhe. Spika, katika jibu lake Mhe. Waziri amesema kwamba uchunguzi wa ajali ya ndege hiyo bado unaendelea. Swali langu.

Je, ndege hii ambayo ilipata ajali imeruhusiwa kuendelea kufanya safari ya kwenda Unguja na Pemba, au imesimamishwa ili kuendelea kujua uchunguzi wa ajali hiyo iliyotokea?

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Naibu Spika, ndege hii haijaruhusiwa na kwa bahati nzuri mimi nilipokwenda Pemba niliwahi kufanya masihara, nikasema angalau kiwanja cha ndege cha Pemba kitalala ndege siku hizi, kwa sababu ndivyo ilivyo, kwa sababu ilikuwa haijawahi kulala ndege. Kwa hivyo, akienda kiwanja cha ndege cha Pemba ataikuta imelala pale.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru kunipa nafasi hii ya kuweza kumuuliza swali moja dogo la nyongeza Mhe. Waziri, ili kuweza kutuelimisha zaidi kuweza kujua masuala haya ya usalama wa viwanja vya ndege pamoja na ndege zenyewe. Swali langu liko hapa.

Mhe. Naibu Spika, tunajua baada ya kutokezea ajali ile kama alivyosema yeye mwenyewe sasa hivi kuna uchunguzi unaendelea na kama alivyoeleza katika suala la msingi kwamba TCAA wao ndio wanaoshughulikia uchungu hiyo ajali ilivyotokezea. Swali langu liko hapa.

TCAA ni chombo cha Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na ile ndege ambayo iliyopata ajali, ilipata ajali katika kiwanja chetu cha Zanzibar kwa upande wa Pemba. Sasa je, hii mamlaka ya TCAA wakishamaliza ule uchunguzi wao ripoti yao itakabidhiwa wapi na ile waziri yeye kama ni waziri ambaye hashughulikii masuala ya Jamhuri ya Muungano.

Je, hiyo ripoti ya ajali ile baada ya kutolewa, sisi hapa kama chombo cha kutunga sheria tutaweza kupata vipi kujua ili tujuwe kwamba viwanja vyetu vina tatizo gani au ndege zetu ambazo tunapanda zina matatizo gani.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Naibu Spika, kama ambavyo nilisema mwanzo. Mhe. Naibu Spika, hii TCAA haitowi ruhusa ya ndege tu lakini hata hivi viwanja vya ndege, kuwepo kwake na kufanya kazi kwake vimepewa leseni na TCAA. Kwa hivyo, wanaweza hata kukifungia kiwanja cha ndege kama hakitimizi yale masharti.

Kwa hivyo, ripoti ambayo wanaitoa inakwenda kwa wahusika, kama ni ndege basi watakwenda kwenye lile Shirika la Ndege, kama ni kiwanja itakwenda kwenye kiwanja. Lakini kama wamezuiliwa leseni wenye kiwanja watajua kwamba ndege fulani imezuiliwa leseni yake, kwa hivyo haiwezi ikafanyakazi, kwa hivyo wao hawawezi wakairuhusu. Lakini hii TCAA inashughulikia usalama wote wa viwanja vya ndege, mazingira yake pamoja na ndege zenyewe zinazoruka ndio kazi yake.

Kwa hivyo, sasa ikiwa Baraza la Wawakilishi inaitaka hii ripoti, naomba niichukuwe kama home work niweze kulifuatilia na Inshaallah tuweze kujua ni vipi itapatikana hii ripoti. (Makofi)

Nam. 76

Wagonjwa Wanaotibiwa Nje ya Nchi

Mhe. Jaku Hashim Ayoub – Aliuliza:-

Kwa kuwa Zanzibar imekuwa ikipeleka wagonjwa nje ya nchi kama vile India, Afrika ya Kusini kwa matibabu kutokana ushauri unaotolewa na madaktari wetu.

(a) Katika kipindi cha mwaka 2010 hadi 2014 Je, ni wagonjwa wangapi wameshapelekwa nje kwa matibabu.
(b) Je, ni nchi gani inatoa matibabu ya gharama nafuu na utaalamu bora zaidi ili iwe kimbilio.

(c) Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kuwa matibabu hayo yote yanafanyika hapa nchini ili kuokoa fedha za kigeni na kupunguza usumbufu kwa wagonjwa.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya - Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 76 lenye kifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Naibu Spika, jumla ya wagonjwa 465 wameshapelekwa nje ya nchi kwa matibabu katika kipindi cha mwaka 2010-2014 na jumla ya shilingi 1,827,347,000 zimetumika, kuanzia mwaka 2010 -2013, na mwaka 2014 hizi bado hesabu zake hazijamalizika, kwa hivyo hizo siwezi kuzipata kwa sasa mpaka tutakapomaliza mwezi huu wa Juni.
(b) Wagonjwa wetu inategemea wapi huduma zinapatikana ambazo hazipo Zanzibar. Kuna wanaopelekwa hapa nchini kwetu Tanzania Bara, pia nje ya nchi, Kenya, India, Afrika ya Kusini, Israel na kwengineko kutegemea wapi shida inaweza kushughulikiwa. Gharama inategemea mgonjwa anatibiwa nini na si pahala anapopelekwa, lakini kutibu mgonjwa hata hapa Zanzibar bado gharama zinatumika.
(c) Serikali ina mpango wa kuleta huduma karibu kwa wagonjwa, ndio mana inaandaa Hospitali ya Mnazi Mmoja kuwa ya Rufaa kwa kuboresha huduma za afya. Madaktari wa fani mbali mbali wako masomoni. Pia timu za madaktari bingwa wenye ujuzi tofauti kutoka nchi mbali mbali zinazokuja Zanzibar, huwa zinapunguza kwa kiasi kikubwa mzigo wa kusafirisha wagonjwa nje. Lakini hiyo haimaanishi kwamba wagonjwa hawatosafirishwa nje, kwani hata nchi zilizokwishaendelea wanatoa wagonjwa kutoka nchi moja kwenda nyengine, ila kwa kiasi tutapunguza idadi ya watakaosafirishwa.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri, kwanza nimshukuru sana kwa kukiri kuwa Hospitali ya Mnazi Mmoja inaandaliwa kuwa hospitali ya rufaa na kuwa bado hatujafikia hospitali ya rufaa, nimshukuru sana Mhe. Naibu Waziri kwa jawabu hilo. Mhe. Naibu Spika, sasa naomba kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali dogo la nyongeza lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Sababu gani zilizopelekea kukosekana kwa matibabu ya wagonjwa, mpaka kusababisha kutumia shilingi bilioni na kidogo kwa gharama za matibabu nje ya nchi.
(b) Mpango wa serikali kuifanya Hospitali ya Mnazimmoja kuzifanya huduma zake kuwa nzuri zaidi na kuifanya kuwa Hospitali ya Rufaa imekuwa ikizungumzwa kwa zaidi ya miaka minne. Je, serikali inatoa kauli gani kuhusu suala hilo.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Naibu Spika, kwa kweli sababu ziko tofauti kulingana na magonjwa tofauti ambayo hayawezi kutibika hapa, yanakosa kutibika kwa sababu ya upungufu wa vifaa, wataalamu pia hatuwezi tukatumia gharama kuwaita madaktari kutoka nje kwa ajili ya kuja kuwatibu wagonjwa hapa. Kwa kweli, hali hiyo ni gharama zaidi kuliko kuwachukua wagonjwa na kuwapeleka pale ambapo una uhakika kwamba watatibiwa na watarudi kwa muda muafaka.

Mhe. Naibu Spika, ili haya yaweze kutekelezeka nayo hayahitaji muda. Kwa hiyo, kumsafirisha mgonjwa itachukua muda mfupi na mgonjwa atapata matibabu kuliko kuyaandaa hayo mengine.

Kuhusu suala la Hospitali ya Mnazimmoja kuwa Hospitali ya Rufaa. Mhe. Naibu Spika, tumesema tunaiandaa kuwa Hospitali ya Rufaa, kwa sababu hayo niliyoyataja mwanzo ya wataalamu, vifaa pamoja na matengenezo yatakapokamilika ndipo itakapokuwa Hospitali ya Rufaa. Kwa hivyo, hivi sasa tuko katika kuandaa na baadhi ya vitu viko tayari, lakini havijatosheleza kukamilisha kusema kwamba hii sasa ni Hospitali ya Rufaa. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, tungekuwa tunazo fedha kama nchi za nje na kwa mfano Bara tu hapo wakitaka Hospitali ya Rufaa kesho iwe basi inakuwa kwa sababu wao fedha wanazo, lakini serikali yetu haijawa na uwezo huo.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Naibu Spika, ahsante sana na mimi kuweza kunipa nafasi hii asubuhi ya leo ya kumuuliza Mhe. Naibu Waziri wa Afya swali dogo la nyongeza.

Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa hivi sasa hatujafikia lengo la kuiita Hospitali ya Rufaa ya Mnazimmoja. Mhe. Naibu Waziri huoni kwamba huko nyuma tulikuwa na lugha ya kusema kwamba ile ni Hospitali ya Rufaa ya Mnazimmoja. Je, haoni kwamba iko haja ya Mhe. Naibu Waziri wa Afya kuendelea kuliita jina hilo.

Vile vile kwa kuwa amesema Mhe. Naibu Waziri wa Afya kwamba vifaa havijatimia na madaktari bado hawajaja. Je, ni lini Wizara ya Afya itaweza kukamilisha, ili kupunguza mabilioni ya fedha ya wananchi kwa lengo la kuwaleta madaktari pamoja na vifaa hapa Zanzibar na kuweza kupata tiba nzuri zaidi.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Naibu Spika, Hospitali ya Mnazimmoja kwa Zanzibar ni Hospitali ya Rufaa, kwa sababu wanaoshindikana Kivunge au Makunduchi ama Pemba wanaletwa Hospitali ya Mnazimmoja. Kwa hiyo, katika nchi yetu Hospitali ya Mnazimmoja bado inabaki kuwa ni Hospitali ya Rufaa. Lakini katika kutibu makubwa bado hatujafikia hatua hiyo na ndio maana maandalizi yanafanywa.

Katika hali hiyo, vifaa vinatakiwa vitumike na madaktari wanatakiwa waelimishwe, kwa sababu daktari haelimishwi kwa mwaka mmoja na wala vifaa haviwezi kununuliwa kwa mwaka mmoja. Kwa maana hiyo, itakapofikia hivyo na ndio maana nilisema kwamba madaktari wanafundishwa na uchache wake ni miaka mitatu kwa hiyo hatuna uharaka tutakaoweza kuufanya kuipunguza miaka mitatu daktari asisome. Lakini pia anaweza kusoma miaka mitatu na ashindwe kukamilisha na pengine inaweza ikamchukua hata miaka mitano kusoma.

Kwa hivyo, haraka ya kusema tutawaleta madaktari kutoka nje hilo haliwezekani kwa sababu tumeshajaribu kuomba, lakini wanachosema wanasema kwamba leteni watu wenu tukufundishieni na halafu waje wafanyekazi na wala hakuna daktari anayetaka kuja, kwa sababu huko kwao waliko nje hawatoshi.

Kwa maana hiyo, uharaka wakusema hilo tutalifanya kwa hayo makubwa ambayo yanatakiwa yafanyike pale basi itachukua muda na ninaomba wastahamili, kwa sababu wanajua na wizara wanaijua kwa mfano juzi wamekataa kupitisha kwa sababu wanasema fedha ni kidogo, sasa sisi tutafanyaje.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Naibu Spika, kwanza ninamshukuru sana Mhe. Naibu Waziri wa Afya kwa majibu yake mazuri na mwanana na leo ametulia sana na ninaamini hata wananchi leo wataridhika sana kwa mujibu ya majibu yanavyotoka. *(Kicheko/Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, jana tulipokuwa tumekwenda kupitia tena hii bajeti ya Wizara ya Afya tulipata taaluma kubwa sana. Kwa hiyo, swali langu lipo hapa kwamba wagonjwa wanaopelekwa nje ya nchi tumekuwa tukilalamika sana kwamba fedha ni nyingi sana ambazo zinazotumika. Lakini tatizo ambalo tumeligundua ni kwamba wale wagonjwa wanaopelekwa nje wakesha kufika kule wanaambiwa baada ya miezi sita warudi tena na hii ndio inayosababisha gharama kubwa sana.

Je, serikali yetu kupitia Wizara ya Afya haioni kwamba ipo haja kwa wale wagonjwa kwa mara ya kwanza wamepelekwa nje na wakaambiwa baada ya miezi sita warudi, wakati ile kazi inayokwenda kufanyika kule pengine haizidi muda wa masaa mawili ambayo hata wao wenyewe Hospitali ya Mnazimmoja wanaiweza.

Kutokana na hali hii Wizara ya Afya haioni kwamba ipo haja kwa wale wagonjwa kabla ya kupelekwa nje kwa ajili ya kwenda kutibiwa wakapewa darasa tosho kwamba si lazima wanapoambiwa warudi tena kule nje, kama vile India au nchi nyengine na wanaweza kupatiwa huduma nyengine hapa Zanzibar, kwa ajili ya kuokoa fedha za serikali au wananchi kwa lengo la kuwapeleka wagonjwa wengi zaidi kuliko ilivyo sasa.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Naibu Spika, kwa kweli hapa kuna vitu viwili ambavyo vinatufunga. Kwanza inaweza kuwa kazi ni ndogo ya dakika mbili, lakini vifaa hatuna vya kuweza kuifanya hiyo kazi ya dakika mbili, kwa hiyo kwa vyovyote inabidi mgonjwa yule arudi kwa ajili ya kwenda kufanyiwa hiyo kazi ya hizo dakika tatu, lakini ndiko atakakoweza kupata matibabu sahihi.

Kwa mfano, tunaweza kuwa na mtaalamu na wanapokwenda kule sisi hatuambiwi kitu kitakachokuja kufanyika mpaka mgonjwa atakaporudi. Kwa hivyo, tunasema yale kwenye *files* na ndicho tunachokijua na kwa wakati ule tunakuwa hatuna uwezo wa kununua hivyo vifaa vya kuweza kuhudumia hayo matibabu.

Jambo la pili ningependa kusema hivi kwamba wagonjwa wanaokwenda wanaambiwa rudi baada ya miezi sita na wakati mwengine wanaambiwa rudi hata baada ya miezi miwili.

Sasa mgonjwa akeshafika India au alikokwenda ameshaambiwa rudi baada ya miezi sita. Kwa hivyo, sijui kwa wagonjwa wetu wa hapa Zanzibar utawaelimisha lugha gani hata waweze kukufahamu aliyeambiwa arudi India umwambie nitakubakisha hapa na sio hao tu, hata hao wenye wagonjwa watapanda wakifuka mpaka iwe tabu na ilhali wanajua kwamba wagonjwa wao wanaweza kutibiwa hapa.

Mhe. Naibu Spika, wakati mwengine tunawaambia Waheshimiwa Wawakilishi hivi vidogo vidogo jamani hapa mbona tunaviweza basi watampandia Katibu Mkuu Dkt. Jidawi mpaka roho itakekumtoka na ilhali akenda kule anaambiwa kila kitu chako kiko sahihi tena ni Waheshimiwa hawa hawa. *(Makofi)*

Kwa maana hiyo, tusaidiane kama kweli mnataka wizara ifanye kazi. Lakini wangapi wameshakwenda huko India na wakarudi hapa hawana tatizo na kama tungeweza kuyafanya hapa kwa ajili ya kuokoa fedha, kwa hiyo si wananchi tu na sisi tuliomo humu ndani tunazitumia fedha vibaya. *(Makofi)*

Nam. 61

Huduma ya '*Outreach'* Kwa Maradhi Yasiyoambukiza

Mhe. Saleh Nassor Juma – Aliuliza:-

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kuthamini afya ya mama na mtoto, imeanzisha huduma ya *'Outreach Services'* jambo ambalo limesaidia sana kwa mama na watoto. Kwa kuwa kwa sasa kunaongezeko kubwa la magonjwa yasioambukiza (*NCD*) hususan kwa watu wenye umri mkubwa, mijini na vijijini, jambo linalotoa usumbufu mkubwa kwa wagonjwa hao.

Je, ni lini serikali itaanzisha huduma ya '*outreach'* kwa wagonjwa wenye maradhi yasio ya kuambukiza (*NCD*) wanaoishi mbali na huduma za afya.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya - Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 61 kama ifuatavyo:-

Inaeleweka kuwa magonjwa yasioambukiza yamekuwa yakitugusa wengi miongoni mwetu, na kwa Zanzibar sasa hivi hakuna familia ambayo haijaguswa na magonjwa haya. Na ndio maana Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Wizara ya Afya imeweka msisitizo maalum juu ya magonjwa yasioambukiza kwa kuyaundia Kitengo cha Maradhi Yasiyoambukiza.

Naomba niseme kwamba huduma za "*outreach*" kwa magonjwa yasioambukiza zimekuwa zikifanyika katika vijiji mbali mbali hapa nchini, isipokuwa kufanyika kwake hakuwezi kulingana na huduma za mama na mtoto ambazo zimeanzishwa takriban miaka 30 iliyopita. Kitengo hicho cha kudhibiti magonjwa yasioambukiza kwa kushirikiana na Timu za Afya za Wilaya (*DHMT*) zimekuwa zikitoa huduma za upimaji hususan wa presha na kisukari pamoja na kutoa na elimu ya afya katika siku ya afya ya vijiji, Maadhimisho ya Siku ya Kisukari Duniani.

Hata hivi karibuni jopo la wanafunzi na wataalamu kutoka vyuo vya udaktari vya Tanzania Bara walikuja kwa ajili ya kutoa huduma hizo. Aidha, kumekuwa na taasisi zisizo za kiserikali kama vile *ZOP* ambazo nazo pia zimekuwa zikitoa huduma hizi katika mtindo wa huo.

Mhe. Naibu Spika, kabla ya hapo wakati tatizo halikuwa kubwa huduma za magonjwa haya zilikuwa zikipatikana katika mahospitali tu. Lakani mpango wa Wizara ya Afya kwa sasa ni kuhakikisha huduma za magonjwa haya zinapatikana kikamilifu katika vituo vya afya.

Lengo ni kueneza huduma hizi katika vituo vyote, lakini kwa kuanzia tutaanza na vituo 34 kwa Unguja na Pemba na hatimaye kuongeza idadi ya vituo kwa kadiri nyenzo zitakapopatikana. Vifaa kwa ajili ya kutolea huduma hizo tayari vimeshafika nchini na ni matarajio yetu, kufikia mwisho wa mwezi huu wa Mei, wafanyakazi wote wa vituo husika watakuwa wamepatiwa mafunzo na kuanza kutoa huduma rasmi.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Naibu Spika, ahsante sana pamoja na majibu mazuri sana yaliyotolewa na Mhe. Naibu Waziri wa Afya naomba nimuulize swali dogo la nyongeza kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa elimu ya afya ni muhimu sana kwa wananchi na kwa kuwa Wizara ya Afya tangu zamani nadhani hadi sasa wanacho Kitengo cha Elimu ya Afya. Je, ni lini kitengo hiki kimepita katika maeneo ya ndani sana ya visiwa hivi vya Zanzibar ikiwemo sehemu ya Umangani, Vumba, Simwambili, Kilimahodi katika Jimbo la Wawi na sehemu ya Bogowa, Kiwani, Nanguji pamoja Kuukuu Kangani kwa ajili ya kutoa taaluma hii hususan kwa vile magonjwa yasiyoambukiza haya hayako *selective* katika masuala ya kula na wala hawaji-*control*.

Je, ni lini kitengo hiki kitapita sehemu za Kuukuu - Kangani pamoja na Vitongoji kule Umangani kwa ajili ya kutoa taaluma ya afya ili wananchi waweze kuona umuhimu wa ku-*control diet* yao pamoja na kufanya mazoezi. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Naibu Spika, Kitengo cha Elimu ya Afya kipo na kinafanyakazi zake vizuri. Lakini Kitengo cha Elimu ya Afya ni kitengo ambacho kinategemea vitengo vyengine. Kwa hiyo, vitengo vile vinashirikiana na Kitengo cha Elimu ya Afya kwa ajili ya kuwaelimisha wao Kitengo cha Elimu ya Afya na halafu kuwaweza wao kupanga mipango, ili waweze sasa kuwasiliana na Mabawana Afya walioko katika wilaya, kwa ajili ya Mabwana Afya wale waweze kutoa taaluma kwa wanavijiji waliopo pale.

Kwa maana hiyo, sio watu wa Kitengo cha Elimu ya Afya watapita kila sehemu kwa ajili ya kwenda kufanya kazi hii, isipokuwa wao wanashirikiana na vitengo na halafu taratibu inaratibiwa na wale Mabwana Afya walioko kwenye wilaya na vituo wao ndio wanaopaswa kupita huko kwenye vituo vyenyewe.

Kwa mfano, akisema kwamba Kitengo cha Elimu ya Afya kiende huko, basi kitahitaji nyenzo nyingi kitu ambacho wao huwa hawana bajeti ya hivyo, kwa sababu bajeti yao inaunganishwa na vitengo.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Naibu Spika, ahsante sana naomba kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa wizara ina mpango wa kuhakikisha huduma za magonjwa yasiyoambukiza zinapatikana katika vituo 34 kama alivyosema Mhe. Naibu Waziri. Je, Unguja itakuwa na vituo vingapi na Pemba itakuwa na vituo vingapi na lini vitaanza kazi.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Naibu Spika, vituo vya *PSU+* ndivyo tutakavyoanza navyo, na katika vituo 34 vilivyoko Zanzibar viko karibu sawa kwa sawa. Kwa hivyo, Pemba na Unguja watapata mahitaji yao kwa usawa.

Lakini hatutaishia hapo isipokuwa tunaanzia hapo kwa sababu jambo ni jipya kwa maana hiyo tunaanza kuwafundisha hao ambao tayari wanavyo vifaa pamoja na madaktari wa uhakika na baadaye elimu hii itasambazwa kwa kila kituo, kwa sababu ni jambo la kawaida na kama tungekuwa na nyenzo basi tungeweza kuwasomesha wote kwa pamoja.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Naibu Spika, ahsante pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba nimuulize swali moja dogo la nyongeza. Kwa kweli Mhe. Naibu Waziri ameeleza kwenye majibu yake kwamba Mabwana Afya wapo kwenye sehemu za wilaya. Hivi Mhe. Naibu Waziri atakubaliana na mimi kwamba Mabwana Afya kwa muda mwingi sana hawafanyi kazi zao ipasavyo kwa mujibu wa sheria zinavyoeleza.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Naibu Spika, siwezi kukubaliana na hilo kwa sababu sina ushahidi.

TAARIFA

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Naibu Waziri wa Afya ahsante sana. Waheshimiwa Wajumbe kabla hatujaendelea tumepata wageni kutoka Skuli ya Sekondari Bububu na jumla yao ni wanafunzi 40 na walimu 5, nawaomba wasimame ili muwaone. *(Makofi)*

Kwa hiyo, karibuni sana, kaeni.

Waheshimiwa Wajumbe, kabla sijamwita Mhe. Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto kwa ajili ya kufanya majumuisho, naomba niwashauri kwamba muda kama huu Waheshimiwa Wajumbe wengi huenda kunywa chai, lakini huwa wakati wa maswali na majibu ama kusomwa kwa bajeti. Lakini leo Mhe. Waziri anafanya majumuisho na mtu akenda kunywa chai akijibiwa hakuwepo hapa, basi hatumpi nafasi ya kuuliza hoja. Kwa hivyo, ninawaomba watu watulie wasikilize hoja tumalize tukanywe chai. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto. Subiri kidogo Mhe. Waziri.

Mhe. Hamza Hassan Juma (Anaendelea) na hata juzi Mhe. Spika alipokuwa akitoa mwongozo kuhusu Wizara ya Afya, aliwaambia kwamba wajiandae kuja kutoa mchango wao siku ya Jumatano, yaani kesho. Sasa hili Mhe. Naibu Spika, nadhani tungelijaribu kuliangalia upya. Kwa sababu inawezekana kuna maoni mengi ambayo atakuja kupigiwa buti Mhe. Waziri, pengine maoni yale kama ingelikuwa yametolewa angekuja kuyapatia ufafanuzi kwa kweli ingelikuwa amepunguza hata zile buti. Mhe. Naibu Spika, naomba mwongozo wako.

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa nimekufahamu. Kwanza Mhe. Hamza Hassan Juma pamoja na Waheshimiwa wengine naomba tufahamiane. Siku moja na nusu tumekubaliana kweli, lakini uchangiaji wetu unakuwa wakati mwengine unavunja moyo. Huku kwenye kitabu cha wachangiaji wote wamemalizika, wamebakia wachangiaji wanne. Hao wanne waliokuwepo juu nitawasoma kama wapo watachangia halafu tutamwita Mhe. Waziri hakuna tatizo. Wachangiaji wanne tu hawa na nawataja kwa majina. Wa kwanza, Mhe. Shadya, wa pili Mhe. Amina, watatu Mhe. Salma na wanne Mhe. Fatma watu wanne ndio waliobakia hao, kwa hivyo nawaita wamalize halafu Mheshimiwa aweze kuchangia.

Mhe. Mahamoud Thabit Kombo: Mhe. Naibu Spika, mimi naomba nikushukuru sana kwa maelezo yako na niombe muongozo wako pia katika ombi hili ambalo nitaliwasilisha kwako, Mhe. Naibu Spika, ililetwa hoja hapa na Serikali juu ya kupunguza dakika iwe dakika 20 badala ya 30, sasa upande mmoja tumekuwa tunawa-*limit* wajumbe katika kuchangia yaani ikifika dakika 20 kama mimi juzi nilikuwa na michango mingi sana katika Wizara ya afya ikabidi mengine niandike kwa maandishi utakuta hoja ile dakika 20 zile unafika na hujamaliza na kikawaida ni dakika 30, lakini baadae tunasema hatuna wachangiaji sasa mimi sioni *logic* kwamba huku tunampunguzia Mjumbe muda wake anakuwa na dakika 20 na upande wa pili tunasema hatuna wachangiaji.

Mhe. Naibu Spika, nakuomba sana kwa heshima na taadhima na kwa unyenyekevu mkubwa turudishe muda wetu ule ule wa dakika 30 na Serikali itoe hoja kwamba turudishe, kwa sababu kama alivyosema Mhe. Hamza tutakuwa hatuitendei haki Wizara husika na pia wananchi wetu hatuwatendei haki, kwa sababu kuna mambo mengi sana ya kuchangia hususan hizi Wizara zinazowagusa jamii moja kwa moja. Mhe. Spika, kwa unyenyekevu sana nakuomba uliangalie hili.

Mhe. Naibu Spika: Ahsante Mheshimiwa kwa kuwa suala lilipita kwenye kamati ya uongozi na kwenye kikao chetu cha pamoja, Spika, anarudi kesho tutakaa nae pamoja tutampa ushauri huo tuweze kutengua kutoka 20 kwenda 30 kikao kiliamua kwa pamoja, kwa hivyo siwezi kuamua mimi peke yangu, tungojee kesho tuite kikao tuamue sote kwa pamoja kwa sababu siwezi kutoa maamuzi peke yangu huo ndio utaratibu, tulikaa kikao tukapendekeza halafu tukaja tukaamua kwa hivyo kikao kile kile kikae tena tutengue halafu tukae hapa tubadilishe, sikuweza kuamua mimi sasa hivi ombi nimelichukua na litafanyiwa kazi.

Mhe. Mahamoud Thabit Kombo: Ahsante Mhe. Naibu Spika, na maelezo yako na nakubali kwamba kikao kilichopitisha ndio kitaweza kutengua hilo nalikubali kabisa, lakini pia tuanaglie *logic* yaani ule uhalisia ulikuwemo humu ndani kwamba kama tumepitisha na kitu tunaona hakifanyi kazi vizuri basi tunaomba tuwasilishe ombi hilo.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Naibu Spika, na mimi niungane mkono na wenzangu waliotangulia, umejaribu kuyataja majini ya waheshimiwa wanne waliopeleka lakini nikuthibitishie kwamba mimi binafsi nilipeleka jana, Mhe. Asha alipeleka jana na kuna wengine hadi hii leo hawajapeleka, kwa sababu utaratibu wetu ni saa moja na nusu, sasa nikuombe kwa busara kwa wale ambao wanataka kuchangia kwa msingi huo kwamba Mhe. Waziri wa Ustawi wa jamii afanye majumuisho jioni. Kwa sababu kuna mambo ambayo kwa kweli tunataka tumshauri Mhe. Waziri kwa ufanisi wa Wizara ya Wanawake na watoto. Kwa hivyo ningekuomba Mhe. Naibu Spika, tuendelee mpaka saa 7.00 ili jioni Mhe. Waziri afanye majumuisho ili upate michango mizuri kwa ajili ya Wizara hii.

Mhe. Naibu Spika: Ombi lako tumelikubali lakini sio mpaka saa saba watamaliza wachangiaji wako wanne wanaotaka wataleta tukimaliza tutaendelea na utaratibu. Kwa hivyo waheshimiwa namuiata Mhe. Amina Iddi Mabrouk, hayupo, kwa hivyo ameshakosa nafasi huyo. Mhe. Shadya hayupo, Mhe. Salma Mussa yupo halafu nawaomba wanaotaka kuchangia walete.

Mhe. Salma Mussa Bilali: Mhe. Naibu Spika, mimi nadhani dakika 20 ulizonipa ni nyingi. Mimi nina mchango mdogo kwa sababu watu wengi wameshachangia lakini kwa kuwa nafasi nimeipata Mhe. Naibu Spika, nitachangia.

Kwanza kabisa na mimi nimshukuru Mwenyezi Mungu Subuhanahu wataala kwa kunijaalia leo kusimama mbele ya baraza lako hili tukufu na kuchangia hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Uwezeshaji, Usatwi wa Jamii Vijana Wanawake na Watoto, lakini pia naomba nimshukuru Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake Wakurugenzi wa Idara zake zote kwa kazi yao kubwa waliyotutayarishia kitabu hiki.

Mhe. Spika, mimi naanza na Idara ya Ushirika naomba kumpongeza kwa dhati Mkurugenzi wa vyama vya ushirika pamoja na watendaji wake kwa kazi yao kubwa wanayoifanya ya ufanisi, pia naomba niipongeze kwa dhati Serikali kwa kuipatia Idara hii Jengo au Ofisi ya kufanyia kazi katika eneo la Migombani. Halafu pia niipongeze Serikali hivyo hivyo kwa kuweza kuwapatia fedha za matengenezo ya Afisi hii, naiomba namuomba Mkurugenzi afanye juhudi za makusudi za haraka haraka ili aweze kuitengeneza Afisi hiyo na waweze kufanya kazi zao kwa ufanisi zaidi.

Mhe. Naibu Spika, naomba niende katika idara ya Mikopo namuomba Mhe. Waziri atakapokuja naomba anieleze katika kiambatanisho Na. 5 cha kitabu chake ameonesha jinsi ya mikopo JK na AK nilipoangalia nimeona kwamba bado kuna fedha nyingi bado hazijalipwa katika mikono ile. Mhe. Naibu Spika, nataka aniambie je, ana mikakati gani ya kuwafuatilia wakopaji wale ili waweze kuilipa mikopo ile na kumalizika kabisa na wengine wapate kukopa.

Mhe. Naibu Spika, pia kuna matayarisho ya mfuko wa uwezeshaji ambao umezinduliwa hivi karibuni, lakini wakopeshwaji wa mfuko huo ni hao hao ambao pengine walishindwa kulipa katika mikopo mingine iliyotangulia. Je, Mhe Spika, nataka Mhe. Waziri aniambie ana utaratibu gani mzuri au amepanga utaratibu gani mzuri ambao utasaidia vikundi ambavyo watakopeshwa kuweza kulipa mkopo huu kwa ufanisi ili na wengine waweze kufaidika.

Mhe. Naibu Spika, nikitoka hapo nakwenda Idara ya Ustawi wa jamii. Mhe. Waziri naomba anieleze ni lini atafanya marekebisho ya wazee wa vijijini kuwarekebishia malipo yao yale ya misaada ili iweze kuwasaidia Mhe. Naibu Spika, fedha wanazopata wale ni chache sana sana kama nilivyochangia katika Wizara ya Katiba ambayo ilieleza kidogo kuhusu misaada ya wazee hawa ilikuwa bado haijafika wakati wake lakini itakapofika nitasema. Kwa hivyo namuuliza tu Mhe. Waziri kwa ufupi kwamba misaada ile baada ya kuwasaidia wale wazee nahisi bado inawazidishia matatizo kwa sababu leo mzee unapomsaidia shilingi elfu tano kwa mwezi, mzee hana uwezo, hana kazi unamzidishia matatizo. Naomba Mhe. Waziri atueleze ana mkakati gani au ana mpango gani wa kuwaenzi wale wazee wa vijijini kama wanavyoenziwa wazee wa mjini wa Sebleni, Welezo na sehemu nyengine kupatiwa makazi na fedha za kuwakimu ambazo zinawasaidia.

Mhe. Naibu Spika, naomba Mhe. Waziri pia anieleze kwa kushirikiana na Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria ni lini hasa wataweza kuwatokomeza hawa vitangi ambao wanatuharibia watoto wetu kila siku, na matatizo haya kila siku tunaeleza. Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya wanawake alileta hapa hoja yake binafsi tumeyazungumza hapa kwa urefu, lakini kila yakizungumzwa tatizo hili linaongezeka siku hadi siku. Kwa hivyo namuomba Mhe. Waziri anieleze ni lini hasa ataweza kuondoa kabisa malalamiko au kupunguza malalamiko ya udhalilishaji ambao unaongezeka siku hadi siku na watoto wetu wa kiume katika jamii zetu.

Mhe. Naibu Spika, pia nilikuwa naomba ufafanuzi wa Mhe. Waziri katika ukurasa wa 79 katika kiambatisho hichi cha ripoti ya kitengo cha *One Stop Centre* Unguja. Kila nikisoma Mhe. Naibu Spika, naona siielewi, ripoti hii inasema kwamba kuna aina ya matukio chini ya umri wa miaka 18 na zaidi ya umri wa miaka 18, wanawake na wanaume.

Sasa ukiangalia hizi takwimu naona haziendi sawa kwa sababu ukisema chini ya umri wa miaka 18, halafu akachanganua wanawake na wanaume lakini idadi inayopatikana haikubaliani na hizi takwimu zilizokuwemo humu, kwa hivyo Mhe. Waziri naomba atakapokuja hebu anipe ufafanuzi, hii ameikosea au ameifanyia kwa makusudi.

Mhe. Naibu Spika, mwisho kabisa kama nilivyosema kwamba mimi sina mengi kwa sababu nilishaona sipati tena cha kuchangia kwa hivyo kulikuwa na mengi ambayo nilikuwa nichangie na nimechangia kwa ufupi ufupi tu, kwa niaba ya wanawake Mkoa wa Kusini Unguja naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Mhe. Fatma Maboruok Said: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi kwa kunipa fursa hii nikachangia machache katika Wizara hii ya Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii Vijana Wanawake na Watoto, kwa kweli kama ilivyojieleza wenyewe kwamba Wizara hii ni ya uwezeshaji ni lazima tuone kwamba ni majukumu makubwa Ustawi wa Jamii inatujumuisha wanawake, watoto, wazee pia vijana ambao ni muhimu kwa wakati wetu huu, kwa sababu wanahitaji mambo mengi.

Mhe. Naibu Spika, nikienda kwenye kitabu hiki niwapongeze sana Idara ya Maendeleo ya Vijana na Wanawake kwa majukumu ambayo mengi na muhimu, kwa kweli jana baada ya kuambiwa kwamba ilikuwa ni mwisho na sisi tupeleke kwa maandishi, kwa kweli nikavunjika moyo na sikuweza kujitayarisha vizuri, lakini hata hivyo nitaweza kuchangia mawili matatu, ili niweze kusukuma hili gurudumu na tuitendee haki kama walivyosema wenzangu tumtendee haki Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake.

Mhe. Naibu Spika, Idara ya Maendeleo ya Vijana ina kazi kubwa ambayo ni kuratibu na kufuatilia utekelezaji wa mpango wa elimu ya stadi za maisha kwa vijana walio nje ya nchi hii. Kama nilivyosema bila ya kuwa na stadi za kimaisha kwa kweli inakuwa ni tatizo kubwa ambalo linawarudisha nyuma lakini kwa kuwa Idara hii inashughulikia suala hili, niwapongeze sana Idara hii.

Mhe. Naibu Spika, vile vile jukumu la kuratibu mbio za mwenge wa Uhuru na wiki ya Vijana kitaifa, pia ninashukuru sana kwa tendo hili kwa sababu Mhe. Naibu Spika, kila taifa lina misimmo yake na mambo yake ya kushajihisha wananchi wake. Niseme kwamba hili ni jambo muhimu kwa vijana kuweza kujua historia na mambo mbali mbali katika nchi yao. Mwenge wa uhuru ni mmoja ambao unahamasisha na kupita maeneo mbali mbali kuhamasisha mambo ya maendeleo. Niseme ni jambo muhimu hasa nikinukuu ule wimbo ambao uliimbwa ambao unasema "*...sisi tunataka kuwasha mwenge na kuweka juu ya Mlima wa Kilimacharo ulete matumaini, pale ambapo pana chuki na palipojaa dharau"*.

Kwa ufupi tu nimesema hayo kwa sababu huu wimbo ni siku nyingi na kwa haraka haraka kuleta heshima pale palipojaa dharau, kwa hivyo niseme Mhe. Naibu Spika, mimi niombe Mhe. Waziri kwamba Idara hii ni Idara muhimu na kwa sababu ina vijana ambao wanataka kuelimishwa juu ya suala hili.

Mhe. Naibu spika, nikienda katika kitabu kikubwa cha bajeti mara nyingi inakuwa sikiangalii lakini pia kitabu hiki nimekitizama kwa haraka haraka, niende kifungu 212100 Mchango halisi wa mifuko ya hifadhi ya jamii, makadirio ya mwaka 2014/15 yalikuwa ni milioni 32. Kwa nini ililikuwa inashuka shuka huu mfuko wa hifadhi ya jamii haukuwa *stable* kutoka 2011/2015. Naomba unapokuja uniambie kwa nini imekuwa ikishuka shuka namna hii.

Mhe. Naibu Spika, kifungu 263100 Ruzuku; kifungu 263120 vile vile nimeona kwamba imeshuka ukilinganisha na mwaka jana kutoka milioni 8.5 mpaka milioni 6.5 na kwa nini pia kifungu 263122 Maendeleo ya Wanawake na watoto 2013/2014 kilikuwa na milioni 9,980,000 na kushuka 2014/2015 na kukisiwa makisio milioni 4,070,000. Mhe. Waziri unambie ni kwa nini vifungu hivi vimeshuka kiasi hicho.

Mhe. Naibu Spika, vile vile kwenye hii *estimate book,* hii kuna Ofisi Kuu Pemba kifungu 21104 malipo ya likizo nimuulize Mhe. Waziri je, wafanyakazi wangapi ambao wapo katika Ofisi ya Pemba lakini kiasi gani ambacho analipwa kila mtu anapokwenda likizo.

Mhe. Naibu Spika, kuna Ofisi Kuu Pemba hiyo pia kuna kifungu 21108 malipo ya kujikimu na malazi 25,000,000 *per diem*, pia naomba Mhe. Waziri atakapokuja anifafanulie kidogo.

Pia Mhe. Naibu Spika, Ofisi Kuu Pemba kifungu 21116 posho la vikao na kamati bajeti yake ni milioni 11,050,000 nimuulize Mhe. Waziri mwaka 2011/2012 kulikuwa na milioni 2,890,000 mwaka 2012/2013 kuna *nil balance*.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Hamza hapa ananambia niseme Kiswahili nasema kulikuwa hamna pesa kuna *zero balance*. Kwa hivyo niseme ni kwa nini vile vile imeshuka na kutoka 2011/2012 ilikuwa na milioni 2,890,000 na 2012/2013 kulikuwa na zero na imeshuka kufikia kutoka samahani Mhe. Naibu Spika, nimeandika mwenyewe kwa sababu nimeandika haraka haraka inani-*disturb* mwenyewe.

Kwa hivyo hapa niseme kwanza hii ninaiwachia na kwa sababu nilikuwa niko katika *process* ya kuandika baada ya kuambiwa kwamba hakuna nafasi tena, nikawa sikuweza kuendelea kwa bahati ilikuwa hata hiyo kuandika kwa maandishi kwa wakati wa jana ningem-*disturb* mwenyewe Mhe. Waziri. Naomba kuunga mkono hotuba hii ya Mhe. Waziri kwa niaba ya wananchi wangu wa Amani.

Mhe. Asha Bakari Makame: Mhe. Naibu Spika, kabla ya yote nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametuwezesha kuwa katika hali ya afya njema. Lakini pia Mhe. Naibu Spika, nichukuwe nafasi hii nimpe pole sana mwenzetu ambaye ni Naibu Waziri wa Wizara ya Elimu kwa kifo cha mama yake. Tumuombee dua Mungu ailaze mahala pema peponi Amina roho ya mama yake.

Sasa Mhe. Naibu Spika, kwanza kabisa nichukuwe nafasi hii ya kumpongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza Mapinduzi kwa kuona kwamba wananchi wa nchi hii wana matatizo mengi ambayo serikali kwa jumla yote hawawezi kuyatatua. Pia nimpongeze Rais kwa kuona mfuko huu wa uwezeshaji kuupeleka pahala ambapo ndipo na ni Wizara hii ambayo ndio inayoweza kuwawezesha wananchi pamoja na vile vitengo mbali mbali ambavyo pia viungane na mfuko huu wa uwezeshaji.

Kwa hivyo mimi niwaombe sana waheshimiwa wajumbe wenzangu, kama kwa kweli hatutomtendea haki Waziri wa wanawake na uwezeshaji kwa ajili ya kumsakama katika mfuko huu wa uwezeshaji wakati mfuko huu ulikuwa mbali lakini amepewa yeye ili kuunganisha na mifuko ile mbali mbali ambayo itawezesha, ili kumsaidia yeye pamoja na watendaji wake kuweka mipango yao mizuri mwanana yenye kuwawezesha wananchi.

Sasa mimi niseme tu Mhe. Naibu Spika, mimi niipongeze sana Serikali hii ya Mapinduzi na hasa kwa sababu inatumia ilani ya Chama cha Mapinduzi. Mimi niombe kwamba si vizuri kila kitu tukasema hakiwezekani au kila kitu tukaisingizia serikali haifanya. Jamani serikali inafanya mengi Mhe. Naibu Spika, kwa hivyo pale serikali inapofanya vizuri basi tuipe haki yake, sio tukae tuseme tu serikali hii wananchi wana hivi, tuipe haki yake kwa kweli ili tuwape moyo wananchi wetu.

Kwa nini nikasema hivyo Mhe. Naibu Spika? Ninasema hivyo kwa sababu baadhi ya wachangiaji wengi sana wanailaumu serikali, serikali ni nani? Serikali ni sisi pamoja na wananchi, sio serikali kwamba imeunda vyombo vya kusaidia, serikali imeunda vyombo vyake imeweka mawaziri, imeweka Manaibu Mawaziri, imeweka watendaji, lakini wa kufanikisha hayo ni sisi kuisaidia serikali. Kwa hivyo niwaombe tu waheshimiwa wenzangu pamoja na yote ni vizuri tukachangia tukamsaidia Mhe. Waziri kuweza kupanga mipango yake mizuri, kwa ajili ya mifuko hii ya uwezeshaji iliyochanganywa pamoja kuweza kufanyakazi zake vizuri.

Mhe. Naibu Spika, nikitoka hapo niende katika unyanywasaji wa kijinsia. Mhe. Naibu Spika, bajeti iliyopita au pakiulizwa masuala mambo haya basi wallahi tunazugumza leo asubuhi ukiamka wameshabakwa watoto 4, 5, maana yake huu mtandao tukisema sisi unafanya kazi yake. Mhe. Naibu Spika, mimi ninaiomba sana serikali iwe makini katika masuala haya. Masuala haya kwa kweli ni magumu mno na niseme kwamba miongoni mwetu ni sisi tunachangia, kama si wewe ni kaka yako, kama si kaka yako ni mjomba wako, kama si mjomba wako ni ami yako.

Kwa hivyo niwaombe tu wenzangu kwamba sisi ndio tunaoishi katika mitaa, tunawajua hawa watu si kwamba hatuwajui, tuisaidie serikali ili hawa watu wasiendelee na vitendo hivi Mhe. Naibu Spika.

Kwa sababu wenzangu wamechangia sana niondoke hapo, nimtahadharishe tu Mhe. Waziri kwamba huu mfuko wa ZAKA naona haukuzungumzwa sijui umehama katika Wizara hii au uko Wizara gani. Nitamuomba Mhe. Waziri aje

anieleze huu mfuko wa ZAKA uko wapi? Maana siku ile tulipozindua, ulizinduliwa huu mfuko wa ZAKA sasa nitaomba labda nimepitikiwa atufahamishe Mhe. Waziri uko wapi huu mfuko, ili nao tuuombe uweko kwake. Kwa sababu tunataka *One Stop Center* ya mambo yote ya wawezeshaji wananchi ili wananchi hawa wasipate shida. Na mimi niishukuru Wizara ya Uvuvi kwa sababu pia kulikuwa na mambo ya kukopa lakini pia yamekwenda katika Wizara hii.

Jengine Mhe. Naibu Spika, niseme tu kwamba Wizara hii ni Wizara nyeti kwa sehemu zote, kwa sehemu ya mama, kwa sehemu ya mtoto, kwa sehemu ya kijamii. Sasa na mimi nimuombe sana Mhe. Waziri kwamba kwa kweli tunaishukuru kwa kuwatengenezea wazee wetu wale ambao waliokuwa hawajiwezi makaazi mazuri na nimpongeze sana Mhe. Waziri katika jambo ambalo analifuatilia. Mojawapo ni hili la kuhakikisha kwamba wazee kwa sababu anajua na yeye atakuwa mzee, anajua kwamba na yeye kazaliwa. Sasa ukimthamini mama wa mwenzio na wewe utakuja kuthaminiwa. Nimpongeze. Lakini sasa niseme kwa zile fedha ambazo anazopewa tuiombe serikali iongeze kidogo fedha zile haziwatoshelezi chochote, wale wazee ambao tunawasaidia.

Nikitoka hapo Mheshimiwa nije katika mambo ya utendaji. Mimi nimshukuru Mhe. Rais, Waziri mwanamke, Katibu Mkuu mwanamke. Afisa Mdhamini wa Pemba ni mwanamke. Hii ni kuonesha kwamba uwezo wanawake tunao, kwa hivyo hapa nimpongeze sana kwa kutenda kazi. Na ni imani yangu kwamba Waziri amepata Katibu mzuri ambae ni mtendaji mzuri, ana uelewa kwa hivyo nitawaomba tu baadhi ya wafanyakazi wenzake, niwombe sana wampe mashirikiano Katibu Mkuu huyu ili kuweza kufanya kazi kwa ufanisi zaidi katika utendaji wa shughuli hizo.

Mhe. Naibu Spika, niseme kwamba sijui Mhe. Waziri aje atueleze hapa hii Mahakama ya watoto maana yake tulisema kwamba huu unyanyasaji umekuwa kwa kweli haungaliwi vizuri hasa katika mambo ya mashtaka haya. Wizara hii ninavyoijua ni kwamba inashirikiana sana na vyombo mbali mbali ambavyo ni vyombo husika. Lakini kuna watu wachache kwa maslahi yao hawawatendei mema watoto wa wenzao lakini watu wanasema mla kuku wa mwenziwe miguu humuelekea. Kwa sababu katika jopo hili la mashirikiano la mambo haya ya unyanyasaji kuna watu wanafanya mbinu makusudi, mtu anagaiwa shilingi 20,000 anaona yeye ndio keshapata ili kufifiliza kesi.

Pia nitoe wito kwa wazazi; wazazi jamani msituvunje moyo wazazi wenzenu, sisi tunapiga kelele kwa unyanyasaji wa watoto wetu lakini baadhi yenu mnaona haya, mnaona haya nini wewe umekaa duniani umekua mpaka umemzaa mwanao umefanikiwa kuzaa, yule mwanao anayeharibiwa, anaharibiwa hazai tena. Wewe umeshakula dunia unamuacha yule mwanao anaathirika wakati wewe dunia umeshakula.

Natoa wito kwa wazazi tuache mambo ya kuona haya, mficha uke hazai tunasema sisi wapemba kwa hivyo tuache kuficha mambo yetu ambayo tunamzidisha yule mtoto ambaye ameharibiwa kumuonea na tunamzidisha kumfanya yeye aonekane si lolote si chochote, asistarehe katika dunia. Kwa hivyo mimi natoa wito kwa wazazi wa kike na wakiume mtoto wako anapofika wakati akanyanyaswa kijinsia basi usione haya kwenda Polisi, wala usione haya kwenda hospitali ndio mambo yalivyo. Kwa hivyo ninaomba sana Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri nimwambie kwamba kwa kweli sisi tuko pamoja nae katika mambo haya ambayo ni mambo yanatuuma kilillahi, si kwamba hayatuumi.

Niwaombe sasa wananchi kwa jumla jamani tuwalinde watoto wetu na mimi niishukuru Wizara ya Elimu kwa sababu tulisema sisi wenyewe hapa kwamba zile *tuition* za majumbani zisiwemo, sasa hivi kuna *tuition* za skuli na mwisho wake ni saa ngapi? Saa kumi na mbili. Kwa hivyo niishukuru sana Wizara ya Elimu katika mazungumzo na kelele tulizokuwa tukipiga wametusaidia na wao.

Sasa niwaombe tu watoto wetu wajaribu sana kujilinda nafsi zao. Wazazi wenzangu tujaribu sana kuwasaidia watoto wetu ili kuwadhibiti na mambo ambayo kwa kweli yatawavurugia katika maisha yao.

Baada ya kusema hayo Mhe. Naibu Spika, nichukue tena nafasi hii nimpongeze Mhe. Waziri na watendaji wake wote lakini niwaombe wajumbe wenzangu wa Baraza la Wawakilishi kwamba tumpe muda Mhe. Waziri hasa katika suala la uwezeshaji ambalo amepelekewa yeye, sasa tumsaidie michango ya kumpa, mipango namna gani ili waweze wananchi kuwezeshwa. Pia niombe sana vikundi vya ushirika, wajiunge pamoja, wajisajili kwa sababu kama hukujisajili basi huwezi ukapata mkopo kwa sababu utakuwa huna muamaala mzuri wa kupewa.

La mwisho ukishakukopeshwa basi ulipe ili iwe ni mzunguko, umekopa wewe ukilipa apate mwenzako.

Baada ya kusema hayo naomba niunge mkono hoja mia juu ya mia ili tumuwezeshe Mhe. Waziri aweze kupitisha bajeti yake hii na kuweza kuifanyia kazi. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Ali Salum Haji: Ahsante Mhe. Naibu Spika, na mimi nikushukuru kwa dhati kupata fursa hii kuweza kuchangia hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii,Vijana, Wanawake na Watoto. Mhe. Naibu Spika, mimi nilikuwa na mambo mawili matatu nilikuwa nataka kuyazungumza.

Suala la kwanza nitoe pongezi kwa wizara kwa kuanzisha kituo cha kutotolea wajasiri amali. Ni jambo zuri na linaleta matumaini kwa vijana wetu na hususan wale ambao wanamaliza ngazi ya form II wakashindwa kuendelea na masomo yao na baadae kubaki mitaani wakawa hawana ajira yoyote. Lakini nilikuwa nitoe tahadhari kwa Wizara; mara nyingi tumekuwa tukianzisha ubunifu wa mambo mbali mbali katika nchi yetu hatimae mafanikio yanakuwa madogo au umalizikiaji wake unakuwa sio mzuri.

Sasa Mhe. Waziri naomba aje atusaidie atakuja kutoa maelezo yake hapa namna walivyojipanga katika kituo hiki cha kutotolea watoto. Labda atueleze wameanzisha utaratibu gani na wanachukua vijana wa ngazi gani. Na hizo ngazi wanazozichukua wanachukua kwa idadi gani na *course* yake itakuwa kwa muda gani?

Pia si tatizo kumchukua kijana ukamuelimisha lakini tatizo lililobakia baada ya kupata taaluma, kupata uwezo wa kutafuta hizo nyenzo za kuweza kufanyia hizo shughuli zenyewe. Kwa sababu ni kawaida iliyojengeka vijana wengi wanapata taaluma mbali mbali lakini matokeo yake wakishapata taaluma uwezo wa kuwa na *fund* wa kuweza kununua vile vitendea kazi akaweza kujishughulisha na zile shughuli zake. Sasa hapa utakuja kunielewesha labda kama kuna mbinu ambazo wameziangalia kupitia mfuko wao; kwamba hawa vijana ambao watatoa wameshamaliza na wameandaa mikakati ya kuwapa mikopo ili waweze kujiendeleza au namna gani ambayo wamehisi wao wataiendeleza kwa kuwapatia taaluma hawa vijana ambao wanategemea kuanzisha hili darasa la itikadi.

Mhe. Naibu Spika, jengine ambalo nataka kulizungumzia ni suala zima la fidia kwa wanaoumia kazini. Hili suala Mheshimiwa limekuwa kama nyimbo, kila siku imekuwa ni tatizo kubwa hata kamati yetu imefanya jitihada ya kukutana na wadau wenzetu wa Wizara ya Fedha wakati wa kulizungumzia suala hili, lakini inaonekana bado ufanisi wake ni mzito.

Mhe. Naibu Spika, hebu mimi nataka tuombe wizara iangalie athari ya mtu anapokuwa ameumia kazini, kwamba anapoumia kazini maana yake huyu mtu anabakia kitandani, na mazingira ya nchi yetu tunaielewa. Kuna mazingira ya mtu kuweza kujisaidia kujitibu lakini kuna mazingira ya mtu anapokuwa yuko nyumbani kuweza kujisaidia kwa kupata maisha. Sasa mtu anapochukua miaka saba au miaka kumi ameumia, anapoa au anaumia anakufa, anapokufa watoto wanakuwa mayatima, fidia haionekani. Kwa kweli hili Mheshimiwa ni suala ambalo linatia unyonge sana. Linatia unyonge, na nimuombe Mhe. Waziri atakapokuja hapa atueleze mpaka muda huu tumefikia wapi katika suala zima la kuwapa fidia wananchi wetu ambao wanapata mitihani ya kuumia katika shughuli zao za kazi.

Mhe. Naibu Spika, jengine ambalo nilitaka nilizungumzie wakati kamati ilipotembelea Hospitali ya Wazee tangu mwaka jana tulikuta kuna tatizo la kutokuwa na uzio kwenye lile jengo, na wazee wetu pale ambao hali zao tunawajua wamekuwa wakilalamika sana, kwani wanakuwa wanaingiliwa na vijana ambao wasiowatakia mema. Vijana wanaingia katika maeneo na wanapoingia katika maeneo wanaleta bughudha, lakini siyo bughudha tu wanafikia pahala pia huchukua baadhi ya mali zao. Kwa sababu wale wazee ni watu wazima, na unajua watu wazima wenyewe wengine hata akili zao inafika pahala inakuwa haziko katika mazingira mazuri.

Sasa mtu anapopata kijipesa chake inakuwa pale chini ya mto inakuwa ndiyo kama benki yao, hivyo vijana wamejenga mazingira ya kuwazoea namna ya wale wazee wanavyohifadhi fedha zao. Kwa hivyo, wanakuwa wanaingia katika majengo na kuwachukulia fedha zao pamoja na baadhi ya nguo zao. Kwa hiyo, hili suala limekuwa kero na limekuwa linapigiwa kelele kwa muda mrefu, na sijapata kujua mpaka sasa hivi wizara ina mpango gani na wamefikia hatua gani katika kuweka usalama wa wazee wetu kule Welezo.

Mhe. Naibu Spika, jengine ambalo nilitaka nilizungumzie halafu niingie kwenye kitabu huku ni suala la mwenge wa uhuru, kaka yangu Mhe. Jussa alizungumzia sana jana. Yeye alijenga hofu ya gharama zinazotumika katika kukimbiza mwenge wa uhuru hapa katika nchi yetu ya Tanzania, na akatoa wazo kwa nini tusitumie njia nyengine za kuweza kuhamasisha shughuli za maendeleo kupitia labda sherehe zetu za Mapinduzi au sherehe za Muungano.

Mimi nataka niseme Mhe. Naibu Spika, suala la kukimbiza mwenge limekuwa kama suala la biashara, na biashara maisha yote unatakiwa utoe ndiyo uingize, kwa sababu tunapokimbiza mwenge shughuli zinakuwa nyingi zinaibuka na wananchi wanapata hamasa. Mimi zaidi nafikiri tuangalie tunachokitoa na tunachokiingiza katika shughuli nzima za kukimbiza mwenge. Tunaweza tukatoa labda milioni 500 lakini tukaingiza karibu bilioni 100. Sasa hili nafikiri ndiyo suala la msingi, sasa nafikiri Mhe. Naibu Spika, bado tunahisi kwamba mwenge wa uhuru unaleta hamasa katika nchi kwenye suala zima la kukimbiza.

Mhe. Naibu Spika, tukibakia katika kuzungumzia suala la gharama ni kwamba tuna mifano mingi tu kama tukijaribu kuiangalia katika suala la gharama basi kuna mambo hata duniani utakuwa huishi maana yake utasema mwisho ukila tu unapata gharama, utasema ule kipande cha ndizi usubiri kesho, lakini tuna kawaida sisi wengine Waislamu tunapoa utasema hata ukifanya ndoa basi wakati wajibu ni kupeana mikono ndoa ikafungwa basi unaweza kusema ukishafungishwa ndoa watu waende zao wasipate hata sadaka. Kwa sababu tunapowapikia vyakula inabidi gharama inakuwa inaendelea na tunafanya mambo mbali mbali, lakini sasa mimi nasema la msingi ni kuangalia gharama tunazozitumia na faida tunayoipata katika suala zima la ukimbizaji wa mwenge.

Hilo ndiyo suala la msingi na mimi nafikiri faida ni kubwa sana, kwa sababu tukija tukiangalia hata wazee watakuja kusema hapo baadae kwamba mwenge wa mwaka jana umeweza kuzindua majengo mangapi, wananchi wamehamasika vipi na majengo yaliyozinduliwa yamesaidia katika hali gani. Sasa nafikiri hilo ndiyo suala la msingi, na siku hizi hata wavuvi wanasema kama hukupeleka chambo basi samaki huwezi ukavua utakimbia kupeleka dagaa, maana yake na dagaa linaweza likapotea likaenda chini likaliwa na samaki usimpate. Lakini nahisi kama ni ishara fulani ya kuweza kuhamasisha wananchi wetu katika suala hili.

Mhe. Naibu Spika, nikitoka hapo nilikuwa nataka nipitie katika vifungu kidogo tu, nina vifungu vyangu kama vitatu ambavyo nimejaribu kuviangalia katika wizara hii.

Mhe. Naibu Spika, kifungu cha kwanza kuna ununuzi wa gari katika ukurasa wa 287, mimi nataka nije nielezwe tu kama hiki hakina gari au wanataka gari ya ziada. Sababu ya kusema hivyo ni kwa sababu ya hofu yangu iko katika fungu 311200 ukurasa wa 287 imetengwa milioni 40,000,000.

Mhe. Naibu Spika, sababu ya kusema hivyo nitakuja kuizungumzia mbele huko halafu kuna fungu ambalo linanipa mashaka mara nyingi hata Mhe. Jussa anapiga kelele sana. Mhe. Naibu Spika, haya masafari namna yanavyowekewa mapesa mengi kupita kiasi, tukawekeza zaidi kwenye masafari tukaangalia maeneo ambayo wakati mwengine yana umuhimu zaidi katika taasisi zetu.

Mhe. Naibu Spika, fungu hili ukurasa wa 288 fungu 220300 mwaka jana safari za ndani na nje zilitengewa milioni 47,960,000 mwaka huu zimeongezeka zinakaribia nusu yake zimefikia hadi milioni 75,870,000.

Mhe. Naibu Spika, fungu la safari limenona kama hivi, lakini kuna mafungu ambayo ndiyo yanasikitisha zaidi kwamba tunawekeza fedha kwenye mafungu ya safari lakini tunapunguza fedha kwenye sekta muhimu za kuwasaidia wananchi wetu.

Mhe. Naibu Spika, ukurasa wa 291 fungu 272100 misaada ya kijamii, maendeleo ya wanawake na watoto. Mheshimiwa fungu hili limepunguzwa kutoka 17,400,000 mpaka 15,410,000, sasa hapa ndiyo tunapopata mashaka Mhe. Naibu Spika kwamba suala la kusaidia maendeleo ya wanawake na watoto hatuyazingatii zaidi tunazingatia zaidi safari za watu kwenda nje. Kutoka milioni 47 safari mpaka milioni 75, lakini masuala ya kuwasaidia wanawake na watoto yamepunguzwa kutoka milioni 17 kuja milioni 15. Sasa hapa ndipo ninapopata mashaka na

mimi katika hili sasa Mhe. Jussa namuunga mkono sana hatuangalii masuala muhimu na ya msingi ya kuwasaidia wananchi wetu. Mhe. Naibu Spika, tunaangalia masuala ambayo labda watendaji zaidi watapata manufaa ya kuhangaika duniani na kupata maposho, ambao wananchi wetu wanaendelea kudhalilika.

Mhe. Naibu Spika, nataka Mhe. Waziri aje kunieleza sababu za kupunguza fungu la maendeleo ya wanawake na watoto kama hawataki wanawake na watoto atakuja kuniambia wakati huo, na hapa nitakuwa mkali sana Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Spika, fungu jengine napata mashaka zile taasisi husika ndizo zilizopunguzwa mafungu. Ukurasa wa 295 fungu 272100 misaada ya kijamii, maendeleo ya vijana Mheshimiwa fungu hili haliniridhishi.

Maendeleo ya vijana ukayatengee milioni 23 lakini safari za viongozi ukaziwekee milioni 75, Mheshimiwa hatutendi haki kabisa. Mhe. Naibu Spika, ni kwamba hatutendi haki na bado hatujawa makini katika kuunda hizi wizara.

Mhe. Naibu Spika, mimi katika watu ambao baadae nitakuja kutoa ushauri kwa Mhe. Rais kuweza kuja kumsaidia Mheshimiwa ili aliangalie kwa makini Mheshimiwa kwa sababu sisi ni binadamu na binadamu yeyote huwa anastahiki kutoa ushauri kwa mtu yeyote. Ni kiongozi wetu mpendwa, mpenda maendeleo, mwenye imani na watu wake lakini nafikiri kuna haja ya washauri kuweza kumshauri zaidi. Hebu haya mawizara tungepunguziwa, Mheshimiwa kuna tatizo? Kuna tatizo yale mapesa ya safari ya kila idara kama tutayachukua bora ziwe idara tatu nchi hii. Mapesa ni mengi lakini mapesa yote yanayokwenda safari za nje, suala la vipando, suala la vikao, maendeleo ni mambo ya msingi hukuti fedha. Sasa nafikiri na hii kuwa na utitiri wa maidara na mawizara ndiyo inatupelekea usumbufu.

Mheshimiwa kama tutakaa tutapata muda wa siku tatu kuliangalia hili buku tukazikusanya labda pesa za safari za idara zote za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na pesa za maposho yote ya idara zote za Serikali ya Zanzibar, mimi nafikiri nchi hii sijui kama hospitali ya Mnazi Mmoja kutakuwa kuna tatizo la vifaa, sitegemei. Kama yale mapesa tutayachukua tuyapeleke pale Mnazi Mmoja sitegemei kama Mnazi Mmoja tutakosa vifaa vya kuweza kuwahudumia wananchi wetu.

Mhe. Naibu Spika: Malizia.

Mhe. Ali Salum Haji: Mhe. Naibu Spika, namalizia kwa huzuni sana namsubiri Mhe. Waziri wangu mimi ni Mjumbe wa kamati yake lakini baada ya kuangalia fungu hili la wanawake na watoto bado napata simanzi, na aje aniambie sababu za msingi za kuja kupunguza mafungu haya na kuongeza mafungu katika masuala ya kununua magari pamoja na safari za nje na ndani ya nchi hii.

Mhe. Naibu Spika, nakushukuru sana.

Mhe. Viwe Khamis Abdalla: Nakushukuru Mhe. Naibu Spika, na mimi kunipa fursa hii nikaweza kuchangia hotuba ya wizara ya mama yangu Bi Zainab Omar. Nichukue fursa hii nimpongeze Mhe. Waziri na watendaji wake wote kwa ujumla jinsi wanavyofanya kazi vizuri na kuweza kuitekeleza ilani ya Chama cha Mapinduzi.

Mhe. Naibu Spika, nianze na mchango wangu juu ya udhalilishaji wa kijinsia kwa wanawake na watoto.

Mhe. Naibu Spika, Wajumbe wengi wameshachangia kuhusu kifungu hiki cha udhalilishaji wa kijinsia kwa upande wa watoto wa kike na watoto wa kiume, udhalilishaji huu unakuwa ukiendelea siku hadi siku.

Mhe. Naibu Spika, hivi karibuni Mhe. Mgeni Hassan Juma ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati hii ya Ustawi wa Jamii hoja binafsi ndani ya Baraza hili tukufu. Mhe. Naibu Spika, hoja hii ilichangiwa na Wajumbe asilimia mia moja ndani ya Baraza hili, lakini Mhe. Naibu Spika, mpaka leo hii hatukupata matumaini yoyote wala hatukupata majibu yoyote kutokana na hoja hii ambayo aliileta Mhe. Mgeni.

Mhe. Naibu Spika, ni kwamba udhalilishaji unaendelea hapa Zanzibar siku hadi siku. Sababu inayofanya udhalilishaji huu uendelee ni kwamba hapa Zanzibar hapana hukumu. Tunatunga sheria na sheria zinapitishwa lakini sheria hazifanyiwi kazi, haiwezekani Mhe. Naibu Spika ikiwa tatizo hili ikawa linaendelea siku hadi siku. Aliyekuwa hana bahati ndiyo anawekwa ndani, aliyekuwa hana mtu ndiye anawekwa ndani, lakini kuna watu hapa wanafanya makosa haya tena ni watu wazima na wana akili zao lakini kwa vile wana pesa eti Mwenyezi Mungu kawajaalia wana pesa, hivyo kesi hizi zikifika Mahakamani zinaliwa na zinaingia kwenye mivungu ya makabati na madroo ya maofisini.

Mhe. Naibu Spika, kesi hizi hazishughulikiwi, ukienda kufuatilia kesi unaambiwa kesi hii haina ushahidi, ushahidi upi huo Mhe. Naibu Spika wakati kila siku watoto wanabakwa na mtoto yule ameshaonekana kama ana kasoro ya kubakwa, na mtoto akibakwa lazima atajulikana huwezi ukasema upate ushahidi. Sasa naiomba serikali kwa kupitia Wizara ya Fedha hiki kipimo ambacho kinatakiwa basi kinunuliwe (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, kwa nini serikali wanashindwa kununua kipimo hiki? Sasa hivi tulikuwa tuna tatizo la meli mbona pesa za kununulia meli zimepatikana, sasa kipimo hiki ambacho ni muhimu katika nchi yetu hii ya Zanzibar mpaka leo hakijanunuliwa, eti tunasema serikali haina pesa, lakini safari za nje wanakwenda siku hadi siku tena viongozi wote, lakini pesa za kununulia kipimo hiki hazipatikani.

Mhe. Naibu Spika, nikitoka hapo niende kwenye Benki ya Wanawake. Benki ya Wanawake ni muhimu hapa Zanzibar kwa sababu benki hii itakapoanzishwa itawasaidia sana kinamama, watapa fursa ya kwenda kukopa kwenye benki yao, watapata fursa ya kujiendeleza na kujiokoa na umasikini.

Mhe. Naibu Spika, nikitoka hapo niende kwenye idara inayoshughulikia mambo ya vijana. Mhe. Naibu Spika, hivi karibuni ndani ya Baraza lako Tukufu tulipitisha mswada wa kuanzisha Baraza la Vijana kwa vile vijana wetu wana matatizo na hawana sehemu ya kupeleka kilio chao, na mswada huo tukaupitisha ndani ya Baraza hili. Kwa hiyo, nimuombe mama yangu Bi Zainab; Waziri wa wizara hii atakapokuja ndani ya majumuisho yake anipatie maelezo ya kina kuhusu Baraza hili la vijana, kwa sababu vijana ndio Taifa kubwa la nchi hii, na vijana ndio nguvu kazi ya Taifa.

Mhe. Naibu Spika, niseme hasa vijana wamenituma kwa sababu toka ilipotamka Baraza hili tayari huu ni mwaka wa nne, tokea Mhe. Rais atamke kuanzisha muundo huu Baraza la Vijana. Kwa hiyo, namuomba mama yangu aje anipatie majibu haya.

Mhe. Naibu Spika, niende kwenye mfuko wa uwezeshaji, mfuko huu wa uwezeshaji wananchi kiuchumi ni mfuko mzuri sana, lakini Mhe. Naibu Spika, mfuko huu mwanzo ulipotolewa watu waliona tu kama pesa hizi ni za serikali tumepewa ili zitusaidie.

Mfuko huu wengi waliokimbilia kuchukua pesa hizi walikuwa ni wanaume, baada ya kupata mfuko huu pesa hizi wengine walienda kuongeza wake. Kwa hiyo, nimwambie mama yangu Bi. Zainab pesa hizi azisimamie kwa sababu ni nguvu za wananchi na wananchi wote wanahitaji kupatiwa pesa hizi ili na wao ziwaendeleze. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, kwa vile pesa hizi wamekusudiwa zaidi vijana, hivyo nimuombe Mhe. Waziri awaangalie vijana zaidi kwa sababu vijana wengi wa Zanzibar hawana ajira, na vijana wako ambao wamesoma na kila siku tutaendelea kupiga kelele na tutasema kama vijana hawana ajira na tatizo lipo linaendelea kukua.

Nafasi za ajira siyo kuwa hamna au siyo kuwa hazipatikani hapa Zanzibar, nafasi zipo lakini nafasi hizi zikishakutoka kijana aliyekuwa hana mtu kwenye serikali basi hapati ajira, kwa sababu kuna tatizo kuna vijana walisomea ualimu tokea mwaka 2008 wenzao wale wale waliosoma pamoja wanawaona wanafanya kazi wameshaajiriwa, lakini wao mpaka leo baadhi yao wako majumbani hawajapata ajira.

Sasa hawa wanaopata ajira zinatokea wapi na tunaambiwa walimu wa masomo ya *arts* hawatakiwi Zanzibar, lakini wako walimu wa masomo ya *arts* hivi karibuni waliajiriwa mwaka jana, japokuwa siyo wizara yako lakini nimeona hapo nigusie kwa vile unashughulikia vijana.

Mhe. Naibu Spika, niipongeze wizara kwa kuanzisha kituo cha *One Stop Centre* katika Wilaya ya Wete, lakini kituo hiki cha *One Stop Centre* kipo na kinafanya kazi zake vizuri, lakini kesi hizi vile vile haziendi, hakuna hata mtu mmoja aliyehukumiwa tokea kuanzishwa kituo hiki cha *One Stop Centre*. Mheshimiwa kupitia wizara yako usichoke jitahidi na Mwenyezi Mungu atakusaidia.

Mhe. Naibu Spika, nimwambie Mhe. Waziri waanzishe kituo hiki Wilaya ya Micheweni kwa sababu tatizo hili limeenea Zanzibar yote, tena wasichelewe kukianzisha kituo hiki huko Micheweni ili watoto wetu watakapofikwa na kadhia hii wapate sehemu ya kwenda kupeleka kesi zao na ziweze kushughulikiwa na kutatuliwa.

Mhe. Naibu Spika, kutokana na mchango wangu huo naomba niunge mkono hotuba hii ya Mhe. Waziri kwa asilimia mia moja, lakini namuomba asichoke kutupatia majibu mazuri.

Mhe. Mussa Ali Hassan: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa kunipatia nafasi ya kuweza kuchangia bajeti hii ya hotuba ya Wizara ya Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto.

Mhe. Naibu Spika, kwa kweli mchango wangu unaanzia ukurasa wa 19 kifungu namba 31 kuhusu ajira kwa vijana. Hivi sasa tuna matatizo makubwa sana kuhusu ajira, vijana wetu wengi wanazurura bila ya kupata ajira yoyote. Hivyo, namuomba Mhe. Waziri atujuilishe amejiandaa vipi katika bajeti yake hii ya 2014/2015 kuweza kuhakikisha kwamba vijana wetu wanapata ajira ama wanapata mikopo, ili kuhakikisha kwamba wanaweza kujiendeleza katika maisha ama kujipatia ajira za kujitegemea. Naomba Mhe. Waziri atapokuja anieleze ni kiasi gani cha fedha ambacho ametenga kuhusu vijana wetu ili kujiimarisha na kuweza kujiajiri wenyewe hasa kwa vijijini wakiwemo vijana wa Jimbo la Koani.

Mhe. Naibu Spika, sasa nichangie ukurasa wa 42 kifungu namba 3 kuhusu kuimarisha hifadhi ya wazee. Kwanza sina budi niishukuru serikali yetu kwa kuweza kuhifadhi wazee wengi hasa mjini Unguja na Pemba. Lakini nimuombe Mhe. Waziri anambie ni mkoa gani wa Zanzibar ambao ameweza kuhifadhi wazee katika nyumba za wazee hivi sasa. Tukiangalia wazee wengi wanatoka mashamba au mikoani na kwamba wanachoka hasa katika mambo ya kilimo, utashangaa wazee wa mjini kwamba wamepata hifadhi nzuri na wazee hao hawajazoea hata kazi za kilimo kama zinazofanywa mashamba. Ni lini atanihakikishia kwamba katika mikoa yetu kutakuwa na nyumba za aina hiyo hasa tukiangalia Jimbo la Koani hatuna nyumba kama hiyo. Naomba akija anihakikishie ni lini tutapata nyumba kama hiyo katika jimbo la Koani, si hivyo mimi nitaondoa shilingi yangu katika bajeti hii. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, nikizingatia kuhusu Mfuko wetu wa *ZACA*. Kwa muda mrefu sana nilizoea katika bajeti hii ilikuwa na fedha zetu za Mfuko wa *ZACA*, lakini katika kitabu hiki leo sikuona Mfuko huo hata sehemu moja ambapo unaendelea kuendelezwa. Nataka nimuulize Mhe. Waziri, huu Mfuko wa *ZACA* umekufa ama upo unaendelea? Kama unaendelea nataka anijuilishe kwa mwaka huu wa fedha kiasi gani ambacho kimetengwa kupata wananchi wetu katika Mfuko huu ambapo pesa hizi zinakuwa hazirejesheki, zinakuwa ni za kuwasaidia wazee pamoja na matatizo yao.

Kwa kweli hivi sasa tuna wazee wengi sana ambao wameshaanza kukaa mjini kuanza kuombaomba mitaani. Siku za Ijumaa imekuwa ni mtindo kwamba wazee wengi wanatawanyika, ingawa kutoa sadaka ni vizuri lakini wakati mwengine mtu anakuomba wakati huna, ukimjibu kwamba sina wazee wengine wanakasirika na siku ya Ijumaa ile anaweza kukuombea dua kutwa nzima usipate pesa. Kuna mpango gani wa kuweza kuwahifadhi wazee hawa ili wasitawanyike kuweza kuombaomba katika maduka hata na watu binafsi.

Hivi sasa ukienda benki yetu wa Zanzibar tayari wameshakaa watu na vikopo vyao chini wanaomba kama vile wale walioko sehemu za Dodoma waliozoea kuombaomba kule mitaani. Ni lini wazee wale wataondoshwa katika sehemu hizo ambazo hivi sasa wameanza kuweka makaazi ya uhakika ya kuweza kuombaomba. Namuomba Mhe. Waziri atapokuja aniambie ni lini suala hili litafutika Zanzibar kabla halijazoeleka. Kwa sababu humo mote walimoendelea kuwemo wameondoshwa, kwa kweli walianza kidogo kidogo kama hivyo walivyoanza hapa Zanzibar, na ukitizama

wenzetu Tanzana Bara walikuwa watu kama hawa ni wengi, lakini waliondolewa wakarejeshwa wote katika mikoa yao hasa Dodoma na sehemu nyengine.

Namuomba Mhe. Waziri atapokuja anieleze lini atawazuia watu wale na kuwajua wametoka katika mikoa gani ili kurudi nyumbani kuanza maisha mapya, hasa ya kilimo na akaweza kuwapatia fedha za kuanzia miradi ya kujitegemea. Kwa kweli Mhe. Waziri hilo ndio tatizo langu kubwa katika wizara hii, kama sitojua mambo haya ambayo nimeyazungumza katika sehemu hii kuwa utayachukulia hatua, si vyema kwamba mimi na wananchi wangu wa Jimbo la Koani kama tutaweza kuipitisha bajeti hii salama.

Mhe. Naibu Spika, kama atayaondoa haya ambayo nimezungumza na atayajibu kama inavyotakiwa, bajeti hii nitaiunga mkono kwa asilimia mia moja. Sasa naiunga mkono kwa asilimia 40 mpaka aweze kunihakikishia kwamba ananijibu, ni lini mambo haya yatatekelezwa katika mikoa yetu ya mashamba pamoja na majimbo yetu ambayo sisi wananchi wa majimbo hayo tunategemea matatizo yakiwepo sisi tunasaidia kwa nguvu zote, lakini mchango mkubwa unatoka katika wizara yake ama mwenyewe Mhe. Waziri, hasa ukiwaona wananchi wangu wa Jimbo la Koani Kisiwa cha Uzi; hivi sasa wanajitegemea kama ulivyoona hivi karibuni wameweza kuleta achari za kisasa, ambapo kiwanda chao kinahitaji kuweza kupata msukumo, ni lini Mhe. Waziri utafika katika kiwanda hicho ili kuwasaidia walemavu wale kuweza kupata maendeleo ambayo yanahitajika.

Kwa hivyo, Mhe. Waziri mimi sitokuwa na mengi isipokuwa nimuombe ahakikishe kwamba haya yote tuliyoyasema ni ya msingi na yanatakiwa kuchukuliwa hatua kwa wakati. Ahsante.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Naibu Spika, nataka nikushukuru na mimi kunipa nafasi hii ili niweze kuzungumza machache ambayo kwa kiasi fulani naamini hata wananchi wangu wa jimbo la Kwamtipura wataamini nimeweza kusimama nikaweza kutetea baadhi ya hoja zao katika wizara hii ya Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto.

Mhe. Naibu Spika, mimi nataka nianze pale alipomalizia rafiki yangu Mhe. Mwakilishi wa jimbo la Kwahani, Mhe. Ali Salum Haji. Alipokuwa akiangalia mafungu na kwa bahati nzuri hata jana tulipokuwa tunaipitia upya bajeti ya Wizara ya Afya tulipokuwa tukiangalia kwenye mafungu, tuliona ni namna gani ya fedha nyingi ambazo tunazipitisha zinakwenda zaidi katika masuala ya utawala, na katika yale maeneo ya huduma pesa zinabakia chache. Lakini mimi nilikuwa najaribu kumwambia tu kwamba Mhe. Ali Salum Haji anataka kufunga banda wakati farasi ameshatoka.

Mhe. Naibu Spika, mimi katika bajeti ya kwanza ya Serikali hii ya Awamu ya Saba, katika bajeti kuu ya serikali nikiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Wenyeviti, ukiangalia kwenye *hansard* nilielezea ni ukubwa wa serikali yetu utaweza kuathiri kiasi gani uendeshaji wa uchumi wa nchi yetu.
Maneno mengi yalisemwa, wengine sijui kakosa hiki, wengine kanuna, wengine kafanya hivi. Mhe. Naibu Spika, leo miaka minne watu ndio kwanza wanataka kufunga banda wakati farasi ameshatoka.

Ukiangalia ukubwa na wingi wa wizara zetu bila shaka na watendaji na madaraka mbali mbali yatagawanyika katika hali hiyo. Mimi nadhani sisi ni sehemu ya ushauri wa serikali, tunajua si rahisi kwa wakati wa sasa hivi kuweza kuzivunja wizara na kuzibana ukazibakisha chache, lakini naamini hili lilikuwa labda ni jaribio tu la Serikali ya Umoja wa Kitaifa, na katika awamu inayokuja tutajaribu kuangalia hata huo Mfumo wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa. Lakini kuwa na mawizara mengi, tukawa na vyeo vingi kuliko zile huduma ambazo zilizokuwa zinatarajiwa, kwa kweli ukiangalia mafungu ya safari lazima yatakuwa mengi.

Kwa sababu kwanza ukiangalia Wakurugenzi wanakuwa wengi, maana jana tulijadiliana sana tukasema hebu tungelijaribu kukusanya hili tabu la bajeti tukaangalia yale mafungu ya mipango na uendeshaji katika masuala mazima ya shuguli za safari mbali mbali. Kwa kweli ni fedha nyingi sana. Kwa hiyo, matokezeo yake katika maeneo ya utendaji ndio utakuta fedha zinakuwa chache.

Kwa kweli watendaji wetu tunawapa pole kwa sababu tunawakabidhi majukumu makubwa, mazito, lakini fedha za kuweza kufanyia kazi zao zinakuwa hapana, na ukiangalia mapato yetu kila siku yanaongezeka. Sasa nilitaka nianzie hapo baadae niendelee katika michango yangu mingine.

Mhe. Naibu Spika, narejea suala langu ambalo karibu miaka minne naendelea kulizungumza, suala la kuwawezesha hasa kinamama kiuchumi. Sisi wengi tumelelewa katika familia za kimasikini kitu ambacho tulikuwa tunakishuhudia katika familia zetu. Baba zetu kitu kikubwa walikuwa wanahangaika kulisha familia, lakini mambo mengine mengi ambayo hasa ya kuwahudumia watoto na mambo mengine mbali mbali mama zetu ndio zaidi waliokuwa wanatushughulikia. Kwa kweli mimi mwenyewe namshukuru sana mama yangu, na namuomba Mwenyezi Mungu ampe afya njema kwa kuweza kunitunza na mpaka nikafikia *stage* hii.

Nilikuwa najaribu kuangalia ni namna gani mama yangu alivyokuwa akipata tabu na anavyotuhangaikia kutuhudumia sisi watoto wake. Kwa hivyo, najaribu kuangalia na ninalinganisha na mama wa watoto wa wenzangu sasa hivi, kwa kweli kinamama hawa wanapata kazi kubwa sana, na wengi wao utakuta wazee wetu hawa hawakubahatika kupata zile ajira rasmi, yaani serikalini. Walikuwa wanaishi katika hali ya kujitegemea wao wenyewe; wanauza kuni, makozi, makaa, urojo, chapati, na maandazi. Na ukiangalia watoto wengi wa Kizanzibari mpaka hao sasa hivi ambao wengine ni wakurugenzi na wengine ni waheshimiwa tuko hapa, basi wamekulia katika maisha ya biashara kama hizo ndogo ndogo.

Mhe. Naibu Spika, mimi katika jimbo langu kuna eneo linaitwa Mboriborini, ukienda pale kuanzia magharibi vibatari chungu nzima, siku hizi pamoja na kuwa kuna umeme lakini mtu ili biashara yake ionekane anaweka kibatari. Wanauza maandazi, chapati, na wengine ukiangalia ni wajane hata waume wa kuweza kuwasaidia hawana, lakini mtu ana watoto sita, saba anawalisha.

Wakati mwengine kinamama hao inafika pahala watoto wanafika kuzuiwa skuli kwa sababu hawana ada, hawana viatu, hawana *uniform*, kimbilio lao huwa wanakuja kwa Waheshimiwa wao hivyo hivyo tunasokotana, tunasaidiana kinachokuwepo. Kwa kweli ndicho kitu ninachokiangalia; kwamba kinamama kama hatujawawekea utaratibu maalumu itakuwa siku zote tunakuja, tunasema na wao wenyewe wataona kama tunaimba tu.

Sasa mimi ushauri wangu, na suala hili katika bajeti iliyopita ambapo masuala haya ya akinamama, uwezeshaji na mambo mengine, masuala ya uwezeshaji alikuwanayo aliyekuwa Waziri wa Kazi Mhe. Maalim Haroun Ali Suleiman. Mimi nilisema sana kuhusu suala la uanzishwaji wa *Women Bank*, yaani Benki ya Maendeleo ya Kinamama.

Suala hili Mhe. Waziri wa Fedha pia na yeye alilitolea kauli, akasema kwamba fedha zinazohitajika ili kuanzisha mtaji wa benki tupate karibu shilingi 15 bilioni, lakini kitu nilichowaambia kwamba shilingi 15 bilioni kile ni kigezo tu ambacho kimewekwa na *BoT* hasa kwa upande wa Tanzania Bara. Kwa sababu *population* ya Tanzania Bara na *population* ya Zanzibar ni tofauti, Bara wenzetu wako 45 milioni sisi tuko milioni moja. Kwa hivyo, mtaji lazima kuwe kuna sera maalum ya kuanzisha benki.

Mimi niliwahi kuwashauri basi serikali katika bajeti inayokuja yaani bajeti hii, serikali ingeliweza kutenga fedha ili ikaweza kuongezewa kwa ajili ya kuanzishwa hii benki ya kinamama. Lakini kwa kweli mpaka leo benki ya kinamama haijaanzishwa.

Mhe. Naibu Spika, mimi natoa ushauri wa bure, sasa hivi Wazanzibari wana pesa, mimi nataka kusema Wazanzibari wana pesa. Pemba mwaka huu uliopita *ZSTC* wamenunua karafuu za shilingi 63 bilioni, Unguja wamenunua karafuu za shilingi bilioni saba.

Mhe. Naibu Spika, tunaiomba serikali itafute fedha ianzishe mtaji wa kuanzisha benki ya kinamama hapa Zanzibar. Mimi ushauri wangu ninaosema serikali watoe fedha nusu yaani tuchukulie watoe fedha karibu shilingi bilioni saba au nane, shilingi bilioni sita zilizobakia ninaamini na sasa hivi kwa bahati Dar es Salaam pale kumeanzishwa soko la hisa, unataka kufungua kampuni au una kampuni yako unaiandikia, ukishakuwa na uhakika wa kutafuta fedha ipo kampuni ya kuweza kuhamasisha kupata hizo fedha za ziada.

Mhe Naibu Spika, wakihamasishwa Wazanzibari naamini hizo shilingi bilioni sita au saba zilizobakia wataweza kununua *shares* ili hii Benki ya Maendeleo ya Akinamama iweze kuanzishwa, na isiwe tu Benki ya Maendeleo ya Akinamama, inaweza ikaitwa Benki ya Maendeleo ya Akinamama pamoja na Vijana.

Mhe. Naibu Spika, tulipokuwa katika safari zetu mbali mbali nje ya nchi tumekuwa tukikutana na wananchi wengi wa Zanzibar. Mfano hata hivi karibuni kuna kipindi ambacho kinarushwa na *Channel Ten* yule Mzee kikofia jina lake kidogo nimelisahau, katika vipindi vyake alirikodi Oman akazungumza na Wazanzibari ambao wako Oman.

Kule wenzetu wanafanya kazi wanapata pesa, wanasema wanatafuta maeneo ya kuweza kuwekeza Zanzibar na wao wakasema hakuna kampuni ambazo tunaweza tukanunua *shares*? Sasa suala la kuanzisha hizi benki si lazima serikali izibebe peke yake, na sasa hivi nafikiri tumeanzisha utaratibu mzuri, tayari tuna sera ya *PPP*, hebu basi sera hii tuitekeleze kwa vitendo, serikali watangaze kwamba kutokana na matatizo ya kinamama tunahisi kuendelea kuwapa mikopo katika vikundi kwanza vikundi vinakuwa vingi, pesa zenyewe zinakuwa kidogo hazitoshi.

Mimi kwa mfano, katika jimbo langu nina vikudi karibu 40, mwaka juzi walipata vikundi vitatu katika vikundi 40 tena vikundi hivyo ambavyo wamejisajili kama vikundi. Lakini kuna wale ambao wajasiriamali ambao wao hawajajianzisha kama vikundi, lakini wanafanya shughuli zao zinaonekana.

Kwa hivyo, kama kungelikuwa kuna benki hii ya maendeleo ya akinamama pamoja na vijana, basi vijana wetu hawa wangelikuwa hawapati tabu, wangelikuwa wanafanya shughuli zao, wanakwenda kufungua *account* pale na *account* za benki kama hizo zinakuwa hazina masharti magumu, huna haja ya kuambiwa sijui weka nyumba, weka nini ili waweze zile biashara zao kuweza kuwa na mtaji wa kila mara.

Mhe. Naibu Spika, Mwezi wa Ramadhani kama huu unaokuja hodi hodi zimeshaanza, wengine wanakwambia maana yake mimi mtaji wangu wa kuni umekufa nataka unisaidie, mtaji wangu wa chapati umekufa nataka unisaidie. Kwa hiyo, kama ingelikuwepo benki hii badala ya mtu kwenda kumpigia hodi Mheshimiwa angelikuwa anakwenda kupiga hodi benki yao wao wenyewe ambayo wangeliweza kusaidiwa katika kuimarisha biashara zao.

Kwa hiyo mimi naomba sana Mhe. Waziri kwa kuwa suala hili la uanzishwaji wa Benki ya Maendeleo ya Kinamama, kwa sababu Serikali ilikwishatoa kauli wamo katika utaratibu, hebu basi aje aniambie huu utaratibu umeweza kufikia hatua gani. Ndio kama nilivyosema kwa kupitia *PPP* mimi naamini Serikali wakitangaza tunaanzisha benki watu wanunue *shares* nadhani wataweza kununua. Hata humu Barazani sisi ndio watu wa mwanzo tutakaoweza kununua hizo *shares.* Kwa sababu humu kuna wanawake ambao wameingia kwa tiketi za Kinamama, wao naamini wangelinunua *shares* nyingi zaidi. Kwa sababu baada ya kuomba pesa zile wapeleke kwenye VIKOBA, sijui kwenye vikundi, pesa zile wangelinunua *shares* ili benki ikawa na mtaji mkubwa na kuweza kuwaendeleza.

Na sisi wengine ambao tuna majimbo ambao kinamama wapo katika majimbo yetu Mhe. Naibu Spika, tungeliweza kununua hizo *shares* ili hii benki ikaweza kuwa na mtaji. Sasa hivi ule wakati kila kitu kufanya peke yako kwa kweli umepitwa na wakati.

Mhe. Naibu Spika, nilisema nichukue muda mrefu kulizungumzia hilo kwa sababu nilihisi lina umuhimu mkubwa sana.

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea nizungumzie suala la Mfuko za *ZACA*. Mhe. Naibu Spika, nikiangalia mfuko huu sitaki niurejee lakini Mhe. Waziri akija nitaomba atoe maelezo. Mfuko wa *ZACA* kwa kweli wananchi walipata fedha.

Kwanza nilikuwa nataka kujua je, mmefuatilia vipi. Ile miradi yao wale ambao mliwapa zile fedha inaendelea vizuri. Na kama haiendelei maana yake mlitwambia kutakuwa na *follow up.* Kwa hiyo tuje tupate taarifa ya wale waliopata Mfuko wa *ZACA* miradi inaendelea vipi, na wale ambao wakae kwa mkao wa kula wa matarajio watakuwa vipi.

Lakini jengine Mhe. Naibu Spika, mimi naomba sana hasa hii Idara ya Mikopo. Katika majimbo yetu Mhe. Naibu Spika, mimi nitatoa mfano katika jimbo langu katika shehia zangu zote tatu, Mkele, Kwamtipura na Shaurimoyo, nina vikundi vingi ambavyo sio kama vikundi kama vile vilivyoanzishwa, kwa sababu kuna pesa, hakuna. Mna

vikundi ambavyo kuna vijana wamejiajiri makapenta wanachonga meza, viti. Basi hebu Mhe. Naibu Spika, aniambie Mhe. Waziri, katika hii mikopo ambayo wameilenga hawa wananchi wangu wa Jimbo la Kwamtipura katika shehia zote tatu. Je, kwa mwaka huu wategemee wataweza kupatiwa mkopo au msaada kiasi gani.

Lakini vile vile nina vikundi vya maseredani. Mhe. Naibu Spika, maseredani mingi mnayopikia majumbani mwenu yanatoka Jimbo la Kwamtipura. Lakini vijana hawa bado hawajawahi kupata mkopo au msaada wowote kutoka katika Wizara hii. Sasa Mhe. Waziri basi hebu akija aje aniambie yupo tayari kufuatana na mimi kwenda jimboni kwangu kuwakagua wale vijana, halafu na yule Afisa wao wa Mikopo ajaribu kunielekeza ni namna gani ataweza kuwasaidia vijana wale. Vipo vikundi vingi, vipo viwanda vingi ambavyo vijana wangu wanaweza wakafaidika.

Lakini jengine Mhe. Naibu Spika, hili nilikuwa naomba sana Mhe. Waziri ashirikiane na Waziri wa Nchi (OR) Kazi na Utumishi wa Umma. Kuna ajira ya utamaduni ya kinamama wetu ambayo wanaifanya katika mahoteli mbali mbali. Kinamama wetu wanapakapaka hina. Mhe. Naibu Spika, sasa hivi ajira zile katika mahoteli mbali mbali badala ya kuwaachia waswahili wakawapaka wazungu hina, leo wanawachukua wazungu waje wawapake wazungu wenzao hina. Hii imetokea wapi? Mhe. Naibu Spika, katika hayo mahoteli na ninazungumza hivi kwa sababu wale zile ajira zao za kuwapaka hina wazungu zimechukuliwa. Naomba nikishamaliza wanitafute kwenye simu ili niwakabidhi Mhe. Waziri kwa kushirikiana na Waziri wa Kazi, ili zile kazi zao zilizochukuliwa na wageni za kupaka hina wazungu, basi warejeshewe wao wenyewe.

Mhe. Naibu Spika, kwa kumalizia nilikuwa nataka niseme kwa ufupi tu haya yaliyobakia ili Mhe. Waziri pengine anaweza akaja akanipa maelezo. Kuhusu suala la *job centre* kwa ajili ya vijana wetu. Lakini vile vile suala la *DNA machine.*

Na hili suala la *DNA machine* Mhe. Naibu Spika, naomba sana Mawaziri wetu wakija waje watupe jawabu za kutosha. Jana tulipokuwa katika Wizara ya Afya kuna mtendaji mmoja alisema kwamba Wizara ya Nchi (OR) Ikulu na Utawala Bora wao katika miradi yao ile ya maendeleo wameweka fungu kwa ajili ya kununulia *DNA machine.* Sasa hili Mhe. Waziri wa Utawala Bora hayupo lakini nilikuwa naomba Mhe. Naibu Spika, kama Waziri anaweza akawasiliana naye tukaweza kujua kwamba kweli hii *DNA machine* inaweza kupatikana.

Lakini vile vile suala la vijana hasa hawa wanaomaliza vyuo kuweza kufungua kampuni zao. Mhe. Naibu Spika, kwa sababu ukiangalia hata nchi za Ulaya sasa hivi kazi nyingi zipo kibinafsi.

Lakini vile vile suala la jela za watoto Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri hili amefanya jitihada gani.

Mhe. Naibu Spika, naunga mkono bajeti hii, lakini zaidi baada ya kupata hasa jawabu ya suala la uanzishwaji wa Benki ya Maendeleo ya Kinamama. Mengine Mhe. Naibu Spika, nitampelekea Mhe. Waziri kwa maandishi na hayo yote nitaomba vile vile yaje yaingie kwenye *hansard.* Mhe. Naibu Spika, nakushukuru.

Mhe. Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwanza nikushukuru kwa kunipatia nafasi hii. Pili, nimshukuru Mwenyezi Mungu *Allah Subhanahu Wataala* kwa kunipa uwezo kwa mara ya pili kusimama ili kutoa majibu kwa maswali mbali mbali niliyoulizwa.

Mhe. Naibu Spika, kwa niaba yangu na kwa niaba ya Wizara ya Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto, napenda kukushukuru wewe binafsi na kuwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu waliochangia Hotuba ya Bajeti moja kwa moja au kwa maandishi.

Jumla ya Wajumbe ishirini na nne (24) walichangia moja kwa moja na Wajumbe wanne (4) walichangia kwa maandishi. Michango yao kwa njia moja au nyengine itaweza kuimarisha ufanisi katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara. Wajumbe wafuatao walichangia katika Hotuba ya Bajeti ya Wizara nao ni:

1. Mhe. Farida Amour Mohammed

2. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk

3. Mhe. Mohammed Haji Khalid

4. Mhe. Marina Joel Thomas

5. Mhe. Subeit Khamis Faki

6. Mhe. Ashura Sharif Ali

7. Mhe. Bikame Yussuf Hamad

8. Mhe. Kazija Khamis Kona

9. Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi

10. Mhe. Salim Abdalla Hamad

11. Mhe. Saleh Nassor Juma

12. Mhe. Salmin Awadh Salmin

13. Mhe. Ismail Jussa Ladhu

14. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu

15. Mhe. Panya Ali Abdalla

16. Mhe. Mohammedraza Hassanali Mohammedali

17. Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa.

18. Mhe. Salma Mussa Bilali

19. Mhe. Fatma Mbarouk Said

20. Mhe. Asha Bakari Makame

21. Mhe. Ali Salum Haji

22. Mhe. Viwe Khamis Abdalla

23. Mhe. Mussa Ali Hassan

24. Mhe. Hamza Hassan Juma

Waliochangia kwa maandishi ni;

1. Mhe. Mahmoud Thabit Kombo

2. Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa

3. Mhe. Shadya Mohammed Suleiman; na

4. Mhe. Asha Abdu Haji

Mhe. Naibu Spika, Wizara inamshukuru Mhe. Farida Amour Mohammed kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Baraza la Wawakilishi ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii, Mhe. Mgeni Hassan Juma pamoja na Wajumbe wote wa Kamati kwa ushauri na miongozo mizuri waliyotupa, na tutajitahidi kuyafanyia kazi.

Pamoja na mambo mengine Kamati imeishauri Wizara kuelekeza nguvu zaidi kwa shamba la vijana lilioko Pemba.Nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wawakilishi kuwa Wizara katika bajeti yake ya mwaka 2014/2015 imeelekeza nguvu zake katika kuliimarisha shamba la vijana lilioko Pemba.

Kuhusu suala la jengo la Idara ya Ushirika. Napenda kumjibu Mhe. Farida Amour Mohammed, Mhe. Bikame Yussuf Hamad, Mhe. Kazija Khamis Kona na Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa ni kweli kwamba Wizara kwa mwaka jana ilishindwa kulifanyia ukarabati. Hata hivyo, Wizara tayari imeweka Bajeti kwa ajili ya shughuli hiyo katika mwaka wa fedha 2014/2015, jengo litafanyiwa matengenezo tena mazuri.

Kwa upande wa suala la fidia, tayari suala hili limefanyiwa kazi kama ilivyoelezwa katika ukurasa wa 47 wa kitabu cha Hotuba ya Bajeti. Wote ambao wanadai malipo yao yapo tayari na utaratibu wa kuwalipa umeanza.

Napenda kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati kwa michango na maelekezo yao.

Mhe. Naibu Spika, napenda kumjibu Mhe. Makame Mshimba Mbarouk suala la Skauti. Wizara itaendelea kushirikiana na Kamati ya kufufua Uskauti ili kuendeleza mafunzo ya kuwajenga vijana katika maadili, ukakamavu na uzalendo wa nchi yao.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk alitaka kuanzishwe chombo cha sheria cha kuwatetea wanawake kupata haki zao, ikiwemo zinazohusu masuala ya kazi. Vyombo hivi tayari vipo ikiwemo Kitengo cha Utatuzi na Migogoro ya Kazi. Aidha, Sheria ya Ajira Nam.11 ya mwaka 2005 imeweka wazi kuhusu masuala ya kijinsia sehemu za kazi na mengine yanayohusu haki za wafanyakazi pamoja na hatua za kuchukuliwa iwapo utatokea ukiukwaji wa sheria hiyo.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Makame Mshimba Mbarouk alitaka pia kujua kuhusu masoko ya wajasiriamali yako wapi. Napenda kwanza nichukue fursa hii nimfahamishe Mhe. Mshimba kuwa tunaposema masoko ya bidhaa za wajasiriamali hatuna maana ya kujenga majengo ya kuuza bidhaa. Lengo hasa lililokusudiwa ni kuwawezesha wajasiriamali kupata fursa ya kuuza bidhaa au huduma zao. Ili fursa hiyo ipatikane kwa wajasiriamali, Wizara huwa inatayarisha mafunzo mbali mbali yenye lengo la kuwaongezea ujuzi kuhusu masuala ya utafutaji soko, ikiwa ni pamoja na mafunzo ya kuimarisha ubora wa bidhaa zao.

Pia Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko huwa inawasaidia wajasiriamali kushiriki katika Maonesho ya Kitaifa na Kikanda ili kupata fursa ya kutangaza bidhaa zao.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu suala la kinamama wanaodhalilishwa kwenye mtandao, hili linasikitisha sana na sote tunapaswa kulikemea kwa nguvu zote. Huu ni udhalilishaji na ni moja kati ya makosa ya jinai na sheria za kushughulikia makosa ya jinai zipo.

Kuhusu suala la mashine ya *DNA*, mhusika sio mimi ni Wizara ya Afya. Mimi sina pesa za kununulia *DNA.*

Mhe. Naibu Spika, nataka nimueleze Mhe. Makame Mshimba Mbarouk kwamba mimi ni Waziri makini na ninayeona mbali, na ndio maana Mhe. Rais akaniamini na akanichagua katika nafasi hii, na ndio maana nikaliona mpaka Jimbo la Kitope. Mimi na yeye tulifuatana alinichukua mpaka Kitope tukafanya mikutano na kadhalika. Huduma zinazotolewa na Wizara zinafika mpaka Kitope. Mfano halisi Vuga Mkadini *SACCOS* kuna vikundi vilivyopatiwa mikopo, kuna Kamati za Udhalilishaji pamoja na Mabaraza ya Watoto. Maeneo niliyoyatembelea ni mengi kwa upande wa Unguja na Pemba, na siwezi kutaja idadi yake hapa hivi sasa, lakini akitaka nitampelekea kwa maandishi.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Mohammed Haji Khalid anaomba watu wa Wilaya ya Mkoani wahamasishwe ili nao waweze kufaidika na mikopo kama zilivyo Wilaya nyengine. Wizara kupitia Idara ya Mikopo imeandaa shughuli ya kuwapatia Masheha wa Wilaya zote kumi za Unguja na Pemba mafunzo kwa madhumuni ya kuutambulisha Mfuko wa Uwezeshaji pamoja na muongozo unaoongoza utoaji wa mikopo hiyo.

Kazi hiyo imeshaanza kwa Wilaya ya Mjini na Magharibi. Na sisi kama Wizara tutapita na tumeshaanza kupita kuwafahamisha watu kwamba sasa hivi kuna mkopo, waje waombe mkopo sio tumlazimishe mtu njoo ukope.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu suala la kwa nini Pemba hawajaajiri wafanyakazi wapya kwa mwaka huu. Napenda kumjibu Mhe. Mohammed Haji Khalid kwamba nafasi zile kumi na tatu (13) zilizoajiriwa Unguja zilikuwa za kujaza nafasi tupu zilizoachwa wazi na wafanyakazi waliostaafu, kuacha kazi au kufariki dunia kwa kipindi hicho. Pemba haikuwa na nafasi hizo ndio maana ikawa hatukuweza kuajiri.

Mhe. Naibu Spika, tunamshukuru sana Mhe. Marina Joel Thomas kwa ushauri wake na tunamuahidi kuwa tutaendelea na juhudi za kupiga vita vitendo vya udhalilishaji wa wanawake na watoto pamoja na aina nyengine zote za udhalilishaji. Tunawaomba Waheshimiwa Wawakilishi mtuunge mkono katika juhudi hizi kwenye maeneo yenu msikae kimya.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Marina Joel Thomas alitaka kujua kuhusu mchanganuo wa fedha zilizochangwa na wananchi wakati wa Mbio za Mwenge kwa mikoa mingine ambayo haijaweka mchanganuo. Wizara ilitoa miongozo kwa Mikoa yote kuweka mchanganuo wa matumizi ya fedha zilizochangwa na wananchi kwa ajili ya miradi ya maendeleo lakini mikoa mengine hawakuleta taarifa zao. Tunamuahidi Mhe. Marina taarifa hizo tutazifuatilia na tutaziwasilisha kwako kwa maandishi.

Mhe. Naibu Spika, aidha, napenda kumjibu Mhe. Marina Joel Thomas suala la vikundi vilivyohitaji mkakati maalum wa urejeshaji wa mikopo, vilitokana na kuwa vikundi hivyo havikurejesha mikopo kwa muda uliotakiwa. Hivyo zamani vilikuwa havikurejesha mikopo ndio maana wakawekewa mkakati maalum.

Mhe. Naibu Spika, namshukuru Mhe. Marina Joel Thomas kwa mchango wake alioutoa kuhusu kupambana na masuala ya udhalilishaji. Kuhusu suala la malezi si la wanawake tu, wala Wizara peke yao, bali ni suala la kila mmoja wetu. Kwa hiyo tushirikiane katika kuimarisha malezi ya watoto wetu.

Mhe. Naibu Spika, pamoja na Waheshimiwa Wajumbe, nataka nimhakikishie Mhe. Subeit Khamis Faki kwamba Wizara bado haijazindua utoaji wa mikopo Pemba. Tulizindua mikopo hapa tarehe 4/06/2014. Na *inshaallah* tutazindua mikopo rasmi tarehe 22/06/2014 tukijaaliwa katika Wilaya ya Micheweni. Tunamuomba yeye na wengine wote washiriki kikamilifu katika uzinduzi huo.

Mhe. Naibu Spika, nakubaliana na Mhe. Subeit Khamis Faki kuwa wazazi na walezi wana mchango mkubwa wa kusababisha udhalilishwaji wa watoto na wanawake. Kwa kuliona hili, Wizara imeandaa mpango wa kutoa mafunzo na elimu ya malezi kwenye familia kwa kuwashirikisha wazazi wanaume na vijana wa kiume katika kuondoa na kuwakinga watoto na udhalilishaji.

Mhe. Naibu Spika, Wizara ina jukumu la kutoa mikopo pamoja na elimu kwa wananchi wenye kipato cha chini kwa Wilaya zote Unguja na Pemba. Hivyo, wananchi hao ikiwemo wa Wilaya ya Micheweni watapata fursa za kuanzisha shughuli za kiuchumi kwa ajili ya kuendesha maisha yao. Tunawaomba Waheshimwa Wawakilishi wasimamie kuona kwamba fedha zinazotolewa kwa mikopo zinatumika ilivyokusudiwa na zinarejeshwa ili ziwasaidie na wengine ili mfuko uwe endelevu.

Kuhusu fedha za michango ya Mwenge. Fedha zinazochangishwa kwa kila Mkoa ni kwa ajili ya miradi ya Mkoa husika tu, hazigaiwi Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar, lakini Mkoa wenyewe unakusanya na baadae zinarudi kwao na zinakwenda kwa wananchi kwa ajili ya shughuli za maendeleo.

Mhe. Naibu Spika, kwa upande wa Programu za Vijana. Vijana wa Zanzibar walipata fursa ya kwenda kujifunza Austria, Misri, Ujerumani, Canada, Msumbiji na Kenya. Aidha, vijana kutoka Japan, Korea, Ufaransa, Ujerumani na Canada walikuja Zanzibar kushiriki katika kazi za kujitolea kupitia mpango wa kubadilishana vijana.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Ashura sharif Ali alitaka kujua kuhusu tofauti iliyojitokeza kwenye makadirio ya mishahara na viwango halisi vilivyolipwa kwa Idara ya Ushirika, Uwezeshaji, Mikopo na Wanawake na Watoto. Tofauti hii inatokana na kuwa makadirio ya mishahara kwa Idara hizo, yamejumuisha na mishahara kwa wafanyakazi wapya waliopangwa kuajiriwa katika mwaka huu. Hata hivyo ajira hizo hazijapatiwa vibali kutoka Ofisi ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma.

Mhe. Naibu Spika**,** Mhe. Ashura Sharif pia alitaka kujua kuhusu tofauti kati ya idadi ya malalamiko yanayohusu wanawake ambapo Unguja yalikuwa ishirini na nne (24) na Pemba tisini na tano (95). Hakuna utafiti uliofanywa, isipokuwa taarifa hizo zinatokana na ripoti zilizowasilishwa katika Idara kwa kupatiwa ushauri, maelekezo na nasaha. Kwa upande wa Unguja, malalamiko huwa yanapelekwa kwenye taasisi za kiraia ikiwemo TAMWA, ZAFELA na Kituo cha Huduma za Sheria.

Mhe. Naibu Spika,napenda kumjibu Mhe. Ashura Sharif Ali kuhusu tatizo la ajira za vijana na wanawake wanaofanya kazi mahotelini, ikiwemo kutopewa mikataba, kufukuzwa kazi ovyo na kunyimwa haki zao. Masuala haya yanasimamiwa na Kamisheni ya Kazi chini ya Ofisi ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma na kuna Sheria inayosimamia masuala haya. Pia masuala ya vyeti vya Watoto na Vitambulisho vya Mzanzibari hayako chini ya Wizara hii.

Aidha, napenda kumjibu kuhusu shamba la Rosela. Vijana hao wamejisajili kama chama cha Ushirika na mapato yanayopatikana katika shamba hilo wanagawana na nyengine kuweka akiba kwa mujibu wa sheria za ushirika. Kila mmoja anapata mgao wake kwa jinsi alivyoshiriki katika uzalishaji.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Ashura alitaka kujua kama Wizara inashirikiana na Wizara ya Biashara na Wizara ya Habari Utamaduni, Utalii na Michezo katika kukuza ajira kwa vijana. Napenda nimfahamishe kwamba Wizara inafanya kazi kwa karibu sana na Wizara zote hizo mbili. Kwa Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko, mashirikiano yetu yako katika kuwapatia taaluma ya utengenezaji na uimarishaji wa ubora wa bidhaa, kusaidia utafutaji wa masoko ya bidhaa zao na kutoa taaluma ya masoko. Kwa upande wa Wizara inayoshughulikia masuala ya Utalii, tunashirikiana katika kuhamasisha vijana kuanzisha shughuli za ujasiriamali katika sekta hiyo na kuwapatia mafunzo ya ujasiriamali ili kuzalisha bidhaa nzuri zitakazokidhi soko la utalii.

Mhe. Ashura Sharif Ali tunakubaliana na suala lako linalohusu udhalilishaji wa watoto wa kiume kuwa limezidi. Hii imedhihirika kutokana na matokeo ya tafiti mbali mbali zinazofanywa na takwimu zinazokusanywa katika vituo vya Mkono kwa Mkono. Wizara hivi sasa imo katika hatua ya kuandaa utaratibu wa kuelimisha jamii kwa kuwashirikisha watoto wa kiume kukataa kudhalilishwa na kushirikishwa katika harakati za kupinga vitendo vya udhalilishaji. Watoto wa kiume nao wasikubali mambo haya, jamani hatari! (*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, kuhusu suala la ukaguzi wa vyama vya ushirika, ni kweli kuwa vinafanyiwa ukaguzi wa kawaida pamoja na ukaguzi wa hesabu, ili kujiridhisha kama vyama hivyo vinaendeshwa kwa mujibu wa sheria na taratibu zilizopo.

Aidha, mwanachama mmoja mmoja anafaidika kutokana na shughuli za kiuchumi wanazozifanya pamoja na mgao wa mwisho wa mwaka kwa mujibu walivyochangia. Aidha, miradi yao ni endelevu na wamepewa mafunzo, elimu ya ubunifu na mbinu za utafutaji soko.

Mhe. Naibu Spika, wazee wanaolipwa shilingi elfu tano (5,000) wanalipwa kupitia Wizara inayoshughulikia masuala ya Tawala za Mikoa. Hata hivyo, suala hili litashughulikiwa zaidi kupitia Sera ya Hifadhi ya Jamii, katika kipengele cha pencheni kwa wote. Kwa taarifa yenu ni kwamba Sera ya Hifadhi ya Jamii ipo tayari tumeshaitayarisha imeshapitia Baraza la Mapinduzi, hivi sasa itaanza kazi zake.

Mhe. Naibu Spika**,** Mhe. Bikame Yussuf Hamad alitaka kujua kuhusu wafanyakazi wawili (2) walioacha kazi. Napenda kumjuilisha kuwa wafanyakazi hao wawili (2) waliacha kazi kwa hiari yao na wameamua kujishughulisha na biashara.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Bikame Yussuf Hamad aliuliza juu ya mradi wa shamba la kilimo cha mahindi cha Nziwanda Micheweni kilichokaguliwa na mbio za Mwenge wa Uhuru lipo hai. Shamba hilo ni la mwananchi na sio la ushirika. Nataka nikuhakikishie Mhe. Bikame Yussuf Hamad kama ulivyouliza ni kwamba shamba hili si la ushirika lakini ni la mtu binafsi. Mwenge wa Uhuru unahamasisha mwananchi mmoja mmoja na vikundi vya ushirika. Inawezekana mtu yeye mwenyewe kakubali kwamba mwenge uende pale ukaone mambo yanayofanywa katika shamba lake. (*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Bikame Yussuf Hamad, kuna mashirikiano makubwa kati ya Wizara na Wizara ya Sheria na Katiba. Kuna kamati inayoshughulikia masuala ya udhalilishaji na ubakaji ambayo Mwenyekiti wake ni Waziri wa Sheria na Katiba na Makamo Mwenyekiti wa Wizara ya Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto. Kwa hivyo mashirikiano makubwa yapo.

Kesi baina ya Wizara ya Katiba na Wizara zinatofautiana kwa sababu Wizara inapokea malalamiko na kuhakikisha kwamba yanashughulikiwa katika vituo vya Mkono kwa Mkono, na zile zinazohitaji kushughulikiwa kisheria zinawasilishwa Polisi na kwa Mkurugenzi wa Mashtaka kwa kuwasilishwa Mahakamani. Kwa hivyo inawezekana huku kukawa kuna mengine na kule kukawa kuna mengine.

Wawakilishi thalathini (30) wa kamati ya kusimamia haki za watoto, wanatoka katika taasisi za serikali na zisizo za serikali. Taasisi hizo ni Wizara ya Elimu, Wizara ya Afya, Wizara ya Katiba na Sheria, Kazi na Utumishi wa Umma, Wizara ya Habari, Jeshi la Polisi, Chuo cha Mafunzo, Mahakama, Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka, Idara ya Ustawi wa Jamii, Idara ya Wanawake na Watoto, *ZAFELA* na *UNICEF*.

Mhe. Naibu Spika Mhe. Kazija Khamis Kona alitaka kujua idadi ya vijana waliowezeshwa kujiajiri. Naomba kumjibu kwamba wizara haitoi ajira ila inawawezesha wanaotaka kujiajiri kwa kupatiwa mafunzo ya ujasiriamali, mafunzo ya ushirika, na mikopo kwa wanaohitaji na kutimiza masharti. Kwa mwaka 2013/2014 vijana 120 wamewezeshwa Unguja na Pemba.

Aidha, alitaka kujua shamba la Tunguu lina vijana wangapi, wametoka wapi na ameshauri mashamba kama hayo yawekwe kila Wilaya. Napenda kumjibu kuwa Shamba la Tunguu lina vijana sita (6) na wametoka katika maeneo ya Fuoni Kibondeni. Wizara imepokea wazo la kuanzisha mashamba hayo kila Wilaya na italifanyia kazi.

Mhe. Naibu Spika, napenda kumjibu Mhe. Kazija vile vile suala lake la riba katika mikopo kwamba iondolewe. Naomba nimuhakikishie Mhe. Kazija kwamba katika mikopo hii tunayotoa ya uwezeshaji wananchi Kiuchumi hakuna riba hata ya senti tano. (*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, kuhusu ajira za watoto, suala hili linashughulikiwa na Ofisi ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma. Hata hivyo, Wizara inatoa taaluma na kuhamasisha jamii na wanafamilia kuhusu madhara ya ajira za watoto na tunashauri warudi Skuli mara moja.

Mhe. Naibu Spika, ninapenda kumjibu Mhe. Kazija kuwa watu sabini na tano (75) Unguja na hamsini (50) Pemba wanaoishi katika mazingira magumu waliotajwa katika hotuba yangu wanalipwa shilingi elfu ishirini (20,000/=) kwa kila mtu ndio tulichonacho sasa, afadhali tuwe na kitu kidogo lakini tugawane kidogo kidogo.

Mhe. Naibu Spika, Hoja binafsi ya Mhe. Mgeni Hassan Juma. Suala hili limeulizwa na Wajumbe mbali mbali, hoja hii inaendelea kushughulikiwa. Baadhi ya kanuni ambazo kwa wakati ule zilikuwa bado hazijatayarishwa sasa hivi zipo tayari zinazohusu sheria ya mtoto zimeshaandaliwa na kuwasilishwa kwa Mwanasheria Mkuu ikiwemo inayohusu uendeshaji wa Mahakama ya Watoto na ya Hifadhi ya Mtoto.

Aidha suala la *DNA* ambalo aliliuliza Mhe. Mgeni Hassan Juma alilizungumzia katika hoja yake binafsi limetolewa ufafanuzi na Wizara husika. Masuala mengine yanayohusu hoja hiyo yanaendelea kufanyiwa kazi.

Mhe. Naibu Spika, napenda kumuarifu Mhe. Kazija kuwa kesi mbili za ubakaji zilizofutwa kwa Unguja ni kutokana na kukosekana ushahidi wa kuwatia hatiani watuhumiwa, na kesi tatu za Pemba zimetolewa hukumu. Kati ya kesi hizo, mbili ni za ubakaji ambapo kesi moja imehukumiwa miaka thalathini (30) na nyengine miaka kumi na tano (15), na moja ni ya kulawiti ambayo imehukumiwa miaka mitano (5).

Mhe. Naibu Spika, napenda kumjibu Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi kuwa, Wizara inakerwa sana na vijana wala unga na wavuta bangi, tunaumia kweli kweli. Suala la vijana ni suala mtambuka linahitaji ushirikiano na taasisi mbali mbali za Serikali na zisizo za Kiserikali. Wizara itaendelea na juhudi zake za kuwapatia mafunzo ya ujasiriamali, mafunzo ya ushirika na kutoa mikopo yenye nia ya kujiajiri na kupunguza umasikini kwa vijana. Waheshimiwa Wajumbe, naomba tushirikiane katika kulitatua suala hili katika majimbo yetu.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi alitaka kujua juu ya aina ya mashirikiano na faida zilizopatikana. Mashirikiano yaliopo ni kushiriki katika mikutano ya Kikanda na Kimataifa inayojadili na kutoa miongozo juu ya masuala ya maendeleo ya wanawake, vijana, watoto, wazee, hifadhi ya jamii na uwezeshaji. Faida zilizopatikana ni pamoja na kujifunza uzoefu katika masuala hayo pamoja na kusaidiwa utaalamu na fedha kwa utekelezaji wa programu mbali mbali.

Mhe. Naibu Spika, napenda kumjibu Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi kuwa, malipo ya fidia kwa walioanguka mikarafuu yanalipwa na Shirika la Biashara la Taifa (*Z.S.T.C.)* sio sisi, na nyumba ya Wazee ya Limbani Pemba itafanyiwa ukarabati, katika mwaka wa fedha 2014/2015. Jumla ya shilingi milioni 50 zimetengwa kwa ajili hiyo.

Mhe. Naibu Spika, napenda kumjibu Mhe Mwanajuma Faki Mdachi kuhusu suala la Wazee wa Makundeni kuwa hawakai katika nyumba za wazee, ni kwamba wazee hao wapo kwenye nyumba zao na kuhusu posho...

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe waliopo nje waingie ndani tunataka tupitishe vifungu.

Mhe. Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto: Wazee hao hawakai katika nyumba zetu wanakaa kwenye nyumba zao, kwa sababu wale walikuja wakaangaliwa na madaktari nao wakasema kwamba sasa wana nafasi ya kurudi majumbani kwao, lakini wakashauriwa wao wenyewe wakasema kwa sababu tumeshazoea hapa Makundeni sisi tunataka tukae hapa hapa kwenye nyumba zetu, kama kuna msaada wowote tusaidiwe. Kwa hivyo tunawasaidia kila mwezi shilingi 25,000/= na wao wapo pale. Kwa hivyo hatujawapeleka kwenye nyumba za wazee Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi.

Aidha, kuhusu suala la malengo kujirejea kila mwaka ni kwamba, hizo ni kazi za Idara ya Ustawi wa Jamii za kudumu, kwani matunzo kwa wazee na watoto wanaoishi katika mazingira magumu yanaendelea na fidia kwa wafanyakazi wanaoumia inahitajika kila mwaka n.k. Malezi siku zote tunalea wazee, kwa hivyo ni lazima isitoke kwenye bajeti yetu.

Vikundi vitatu vya Mkoani vilivyopatiwa mikopo ambavyo Mhe Mwanajuma Mdachi alitaka kuvijua ni:- Chokocho kimoja na Chambani viwili. Na kuhusu mikopo 550 imetolewa wapi, naomba aangalie kiambatanisho namba 4 ukurasa wa 74. Mambo yote hayo yamejieleza lakini Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi nakuomba usivunjike moyo mikopo tumeizindua juzi. Kwa hivyo una nafasi ya kusimamia watu wako kuja kuomba mikopo katika wizara ya mikopo.

Aidha napenda kumueleza Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi sehemu zenye kesi nyingi za kubakwa na kukashifiwa ni maeneo ya Fuoni na Mwanakwerekwe kwa Mjini/Magharibi Unguja. Hayo ndio stadi hasa, sisi tukizungumza siku ya pili watoto wanabakwa.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Salim Abdalla Hamad alitaka kujua maana ya UVIKIUTA, asili yake na inafanya shughuli gani hapa Zanzibar. UVIKIUTA ni Ushirika wa Vijana wa Kikiristo na Uzalishaji Tanzania. Ushirika huu unashirikiana na vijana wa Zanzibar na wa mataifa mengine kufanya shughuli mbali mbali za maendeleo katika jamii kupitia makambi ya vijana.

Mhe. Naibu Spika, napenda kumjibu Mhe. Salim Abdalla Hamad kuwa uandaaji wa miongozo ya viongozi wa dini ya kupinga vitendo vya udhalilishaji wa kijinsia imeshirikisha viongozi wa dini zote mbili pamoja na Ofisi ya Mufti. Miongozo hii imekusanya aya za Qur-an na hadithi tofauti pamoja na maandiko ya Biblia inayopinga vitendo vya udhalilishaji wa kijinsia ili kuwarahisishia viongozi wa dini hizo kufanya rejea wanapofanya mihadhara na mahubiri katika jamii.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu tathmini ya sheria ya ndoa imefanyika kutokana na kuwa sheria hii imepitwa na wakati na hivi sasa kuna wimbi kubwa la talaka, kutelekezwa wanawake na watoto na pia watoto kukosa matunzo. Malalamiko mengi ya aina hii yanakuja Wizarani, hivyo ilionekana ni vyema sheria hii kufanyiwa marekebisho. Sheria hii itahusisha masuala ya ndoa kwa dini zote. Lengo ni kuhakikisha kuwa haki za wanawake na watoto zinapatikana. (*Makofi*).

Aidha, tunapozungumzia usawa wa kijinsia, tunamaanisha kuwa wanawake na wanaume wapate fursa sawa katika nyanja zote ikiwemo za kisiasa, kiuchumi, na kijamii kama vile fursa za ajira, mikopo, ushiriki na ushirikishwaji katika vyombo vya maamuzi n.k. Namhakikishia Mhe. Mjumbe kwamba yanayohimizwa katika dhana hii ya usawa wa kijinsia hayaendi kinyume na miongozo na maadili ya dini.

Mhe. Naibu Spika. napenda kumjibu Mhe. Salim Abdalla Hamad kuwa Wizara ina jukumu la kuhamasisha vijana kujiajiri, hivyo ushauri wake wa kuongeza juhudi na kuwapa vipaumbele vijana tunauthamini na tutaufanyia kazi kwa kushirikiana na taasisi zote zinazozalisha ajira.

Vile vile napenda kumjibu Mhe. Salim kwamba watu wote wanaodai fidia ni thamanini na tisa (89), Arubaini na moja (41) Unguja na Arubaini na nane (48) Pemba. Watu wote hao watalipwa akiwemo Bibi Asha Rubea Hafidh ambaye ulimtaja.

Mhe. Naibu Spika, pia napenda kumjibu Mhe Salim Abdalla ambaye alitaka kujua kwa nini baadhi ya Wilaya zina mikopo mingi, lakini fedha za mikopo hiyo ni chache, na Wilaya nyengine zina mikopo michache lakini fedha zilizotolewa ni nyingi.

Wingi au uchache wa fedha za mikopo unategemea aina ya biashara iliyoombewa mkopo, na kiwango cha mkopo kwa biashara husika. Kuhusu mikopo ya AK na JK, kwa sasa inasimamiwa na Wizara, na fedha zake zimeunganishwa katika Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi kiuchumi usiwe na wasi Mhe. Salim Abdalla Hamad mikopo ndio kwanza tunaianzisha sasa hivi.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, napenda kumpongeza Mhe. Saleh Nassor Juma kwa michango na pongezi alizozitoa na nimhakikishie kuwa, Wizara haichagui wapi pa kutoa mikopo ilimradi taratibu ziwe zimefuatwa. Aidha, Wizara itawasiliana na kikundi cha Udusini ili kipatiwe miongozo ya kupatiwa mikopo, na kama wataihitaji waombe. Kikundi cha kibokoni tayari tumeanza kufanya nacho kazi kwa kukipatia mafunzo.

Mhe. Naibu Spika, napenda kumjibu Mhe. Saleh Nassor Juma suala lake linalohusu usajili wa vyama vya ushirika. Kuhusu usajili wa kikundi cha kuvunja kokoto tutakifuatilia na kuwaelekeza utaratibu ili wapate usajili, na kuhusu suala la mfanyakazi wa nyumba ya Wazee Limbani Pemba, tayari ameshakabidhiwa Vespa kwa kazi zake, sijui kaifichia wapi, anajitembeza kwa miguu, lakini zamani Vespa anayo.

Mhe. Naibu Spika, napenda kumjibu Mhe. Salmin Awadh Salmin, kuwa sera zote kwa mujibu wa taratibu zinathibitishwa katika Baraza la Mapinduzi. Sera ya Hifadhi ya Jamii tayari imeshapitishwa na Baraza la Mapinduzi na iko tayari kwa kufanyiwa kazi.*(Makofi)*

Kuhusu watu waliopewa mikopo Wilaya ya Mjini, wamo pia watu wanne (4) kati ya hamsini na nane (58) wa Jimbo la Magomeni wamo. Aidha, tunashukuru ushauri uliotolewa na Mhe. Salmin Awadh na tutaufanyia kazi.

Mhe. Naibu Spika, sasa naomba kumjibu Mhe. Ismail Jusa Ladhu, kuwa vipaumbele vya Wizara hii ni; kuimarisha Programu za Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi, Hifadhi ya Wazee na wananchi wanaoishi katika mazingira magumu zaidi, maendeleo ya vijana na wanawake, mapambano dhidi ya udhalilishaji wa wanawake na watoto, pamoja na kushajiisha usawa na uwiano wa kijinsia, kama ilivyoelezwa katika ukurasa wa tano (5) wa kitabu cha hotuba ya bajeti ya Wizara. Hata hivyo, napenda nitoe ufafanuzi kwa vifungu alivyovitaja kama ifuatavyo:-

Fungu la safari limeongezeka kutoka shilingi 15,000,000/= mpaka 25,302,000/=, kutokana na kuongezeka kwa mahitaji ya wafanyakazi wanaposafiri, kushiriki vikao mbali mbali kama vya kamati tendaji, lazima waliokuwa Pemba waje kwenye vikao vyetu vya kamati tendaji, kamati ya uongozi lazima waje, vikao vya bajeti lazima waje, vikao vya kuripoti utekelezaji wa kazi na ufuatiliaji mishahara kila mwezi lazima waje, pamoja na ongezeko la idara

tatu katika muundo wa wizara. Maana sasa hivi kuna ongezeko la idara tatu, kuna mikopo, kuna ushirika na kadhalika. Kwa hivyo, ndio maana hiki kifungu kikawa kikubwa zaidi Mhe. Ismail Jussa Ladhu.

Fungu la Mafuta na Vilainisho limeongezeka kutoka shilingi 20,087,000/=, mpaka 31,634,000/=. Hii ni kutokana na kuongezeka kwa gharama za umeme, maji na mafuta, pamoja na ongezeko la vifaa vya usafiri. Gari moja na vespa sita kutoka Idara tatu zilizoongezwa katika muundo mpya wa wizara, na kama hatuna usafiri je, tutawafikia vipi wananchi?

Vifaa na huduma za ofisi vimeongezeka, kutoka 12,770,000/=, mpaka kufikia 24,355,000/=. Fedha hizi ni kwa ununuzi wa *stationaries* na vifaa vyengine vya kazi, ambavyo vinatumika kila siku na vimepanda bei kaka yangu. Aidha, ongezeko kwenye fungu hili limetokana na ongezeko la mahitaji kutokana na kuongezeka kwa idara tatu katika muundo mpya wa wizara.

Ruzuku Maendeleo ya Wanawake na Watoto. Fedha nyengine kwa shughuli za maendeleo ya wanawake na watoto zimewekwa katika fungu la kusaidia shughuli za kiuchumi na kijamii. Fungu namba 272109 ambapo kuna jumla ya shilingi 5,935,000/=.

Kifungu cha Mwenge wa Uhuru kimeongezeka kutoka 3,610,000/= mpaka 6,343,000/=. Hii inatokana na umbali wa pahala kunakozinduliwa Mwenge. Kwa mfano kama mara hii Mwenge umezinduliwa Bukoba, watu wamepanda ndege mbili, kutoka hapa sijui mpaka Mwanza na Mwanza mpaka tukafikia Bukoba. Kwa hivyo, lazima fungu hili liwe kubwa. Mwaka jana uzinduzi ulikuwa Pemba, hivyo gharama zilizotumika zilikuwa chini ukilinganisha na mwaka huu, ambapo uzinduzi na kilele utafanyika katika Mikoa ya Tanzania Bara.*(Makofi)*

Idara ya Mikopo. Fungu la viburudishaji limeongezeka kutoka 9,290,000/= mpaka 12,760,000/=. Gharama hii inahusisha viburudishaji katika mikutano juu ya uelimishaji wa taratibu za uombaji mikopo, kwa Mfuko wa Uwezeshaji katika Shehia za Wilaya zote za Unguja, vikao vya kuidhinisha mikopo na shughuli za mafunzo kwa wakopaji. Maana lazima tuwafanyie mafunzo, wengine hawajui, kama watu hukuwafanyia mafunzo itakuwa mambo hayaendi.

Kifungu cha Sera na Sheria kimetengewa jumla ya shilingi 25,455,000/=. Fedha hizo ni kwa ajili ya kuandaa mipango ya Utekelezaji wa Sera ya Hifadhi ya Jamii, ambayo sasa hivi tumeshaitayarisha nayo iko tayari kwa kuanza kazi. Sera ya Uwezeshaji, pia Sera ya Maendeleo ya vijana na Sera ya Watoto. Sera tatu hizo ni lazima tuwe na pesa za kutosha. *(Makofi)*

Fedha za huduma za utafiti shilingi 33,255,000/=. ni kwa ajili ya kufanya utafiti wa kuangalia athari za utalii na mmongonyoko wa maadili kwa vijana. Matumizi ya fedha hizi ni pamoja na malipo ya mtaalamu muelekezi, ukusanyaji wa taarifa na uandaaji wa ripoti. Ni lazima tunahitaji tupate mtaalamu muelekezi na kama hatujampata mengine yatatushinda.

Kuhusu shilingi 1,200,000/= kwa ajili ya mikutano ya ushirikiano wa kimataifa, fedha hizi zitatumika kugharamia mikutano ya ndani ya mashirikiano na washirika wa maendeleo. Mikutano hiyo ni kwa ajili ya kutathmini utekelezaji wa programu mbali mbali za wahisani zinazotekelezwa na wizara.

Idara ya Maendeleo ya Wanawake na Watoto. Fungu la safari limeongezeka kwa shilingi 1,800,000/= kutokana na mahitaji halisi ya gharama za safari za kazi nje ya nchi. Hii ni pamoja na kushiriki katika mikutano inayojadili masuala ya watoto na wanawake ambayo inafanyika kila mwaka. Tunatakiwa lazima twende kwa sababu na sisi tumo huku Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, fungu la misaada ya kijamii. Tofauti baina ya Pemba na Unguja, inatokana na tofauti katika idadi ya wazee, ambapo Pemba kuna wazee wanane (8) na Unguja (56) ambao wanapatiwa huduma mbali mbali ikiwemo chakula, nguo na posho.

Idara ya Uendeshaji na Utumishi. Fungu la safari limeongezaka kutoka shilingi 10,320,000/- hadi shilingi 43,800,000/-. Ongezeko hili linatokana na mahitaji halisi ya safari za kikazi ndani na nje ya nchi, kwa viongozi wakuu wa wizara. Mimi natakiwa niende Marekani, pamoja na kuogopa ndege lakini natakiwa niende Marekani na nauli sio ndogo. Kwa hivyo, ikiwa nauli sio ndogo lazima pesa ziwe nyingi, tena sio niende mimi tu, anatakiwa na

Katibu Mkuu na Manaibu Katibu Wakuu, wote tufuatane kwa pamoja. Hii ni pamoja na kushiriki mikutano ya kimataifa na kikanda inayohusu shughuli za wizara.

Fungu la viburudishaji limeongezeka kutoka shilingi 5,750,000/ kutoka 11,900,000/-. Ongezeko hilo linatokana na mahitaji halisi ya uendeshaji wa vikao mbali mbali vya wizara, ikiwemo vikao vya kamati ya uongozi wa wizara, kamati ya ukaguzi, bodi ya zabuni pamoja na vikao na wadau mbali mbali wa wizara. Bajeti iliyotengwa mwaka jana ilikuwa pungufu hata maji tulikuwa hatupati kulingana na mahitaji halisi. Kwa hivyo, jamani tukae kwenye vikao kutwa basi hata maji tusinywe? *(Makofi)*

Fungu la mafuta na vilainisho limeongezeka kutoka 28,270,000/- mpaka 58,795,000/-. Hii ni kutokana na kuongezeka kwa mahitaji kutokana na kuongezeka kwa Idara tatu katika muundo mpya wa wizara, sambamba na kuongezeka kwa vyombo vya usafiri. Pia, fungu hili linahusisha gharama za umeme na maji ambazo nazo zimepanda.

Kifungu cha huduma za mtandao wa Serikali (*E. Government*) mwaka huu kimetengewa shilingi 20,000,000. Mwaka jana shughuli hii haikufanywa kutokana na kukosekana kwa fedha.

Katika matumizi mengineyo kilichopandisha idadi ya fedha ni kifungu cha huduma cha mkataba chenye shilingi 6,000,000/=. Fedha hizi zinakusudiwa kulipia huduma za ulinzi wa jengo la wizara ambalo limekaa katika mazingira hatarishi kiusalama.Mwaka jana wizara ilikuwa katika jengo jengine ambapo huduma hii haikuhitajika, lakini sasa hivi tuko kwenye huduma nyengine, lazima huduma hii ipatikane.

Kuhusu kifungu cha miradi ya maendeleo katika mwaka wa fedha 2014/15, wizara itatekeleza miradi minne (4) ambayo uchambuzi wake ni kama ifuatayo:

1. Mradi wa hifadhi ya wazee wenye shilingi 50,000,000 ambazo zimekusudiwa kutumika kwa ukarabati wa nyumba ya wazee Limbani na kufanya utambuzi wa wazee ili kujua idadi yao halisi na mahali walipo kwa lengo la kuimarisha huduma zao.

2. Mradi wa kuanzisha kituo cha kutotoa wajasiriamali wenye shilingi 200,000,000/- ambazo zitatumika kwa ununuzi wa vifaa na samani, kufanya ukarabati wa jengo la kituo hicho pamoja na kugharamia huduma za mawasiliano na utawala.

3. Mradi wa kuanzisha chuo cha kuwafundisha wanawake kutengeneza umeme wa nishati ya jua na elimu ya ujasiriamali wenye shilingi 400,000,000/-. Fedha hizo zitatumika kwa ukarabati wa jengo. Vijana wetu tuliowapeleka India wamekwenda kusoma wamerudi, sasa wanataka kazi ile wailete hapa. Lazima kwa vyovyote tutumie pesa nyingi kukarabati majengo, ili watakapokuja mambo yetu yaonekane kwamba tumetia mkazo katika kufuatilia jambo letu.

4. Programu ya Ajira kwa Vijana yenye shilingi 874,000,000/-. Shughuli zitakazotekelezwa ni pamoja na ununuzi wa boti moja kwa kuwafundisha vijana uvuvi wa bahari kuu, mradi wa ufugaji wa kuku na nyuki kwa vijana, uimarishaji wa mashamba ya vijana ya maua na mboga mboga, Tunguu; Unguja na Mbuzini; Pemba na ununuzi wa vifaa kwa ajili ya kuwasaidia vijana kujiajiri katika ukusanyaji taka. Sisi hatuna ajira lakini tunawasaidia vijana ili waweze kujiajiri wenyewe.

Mhe. Naibu Spika, napenda kumjibu Mhe. Ismail Jussa Ladhu kuhusu faida za Mwenge wa Uhuru kwa wananchi wa Zanzibar. Mwenge wa Uhuru ni chombo kinachotumika kama ni moja ya alama ya Tanzania inayotumika katika vyombo vya Ulinzi na Usalama, elimu na hata Benki Kuu.

Dhana mpya ya Mwenge wa Uhuru ni kuhamasisha maendeleo kupitia miradi ya kijamii katika wilaya. Aidha, Mwenge wa Uhuru unatumika kuhamasisha umoja, amani na utulivu katika nchi yetu, pamoja na kuelimisha wananchi mambo mbali mbali kama vile mapambano dhidi ya UKIMWI, dawa za kulevya, rushwa na malaria. Hiyo ni kazi ya Mwenge wa Uhuru. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, namshukuru Mhe. Hussein Ibrahim Makungu kwa ushauri wake na pongezi alizotupa. Kuhusu suala la masharti ya mikopo alilouliza Mhe. Makungu, hili tayari limezingatiwa katika muongozo wa Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi.

Aidha, tunamshukuru sana kwa msaada wake alioahidi wa kutoa gari kwa ajili ya kuwatembeza wazee wanaoishi katika makao ya Wazee Sebleni na Welezo. Sisi tumeshindwa, lakini Mhe. Hussein Ibrahim Makungu anataka kutusaidia, nampongeza sana. Tunawaomba na Wajumbe wengine waoneshe moyo kama huu wa kizalendo, tusaidie vijana wetu jamani tusiwaache nyuma.

Mhe. Naibu Spika, napenda kumshukuru Mhe Panya Ali Abdalla kwa ushauri wake alioutoa kwa wizara na tunamuahidi kwamba tutaufanyia kazi. Aidha, ombi lake la kuvitembelea vikundi vilivyokuwa havijatembelewa nimelipokea na nitalifanyia kazi kadri wakati utakaporuhusu, nitakapojaaliwa *Inshaallah*, tutaifanya kazi hii kwa pamoja.

Mhe. Naibu Spika, napenda pia kumshukuru Mhe. Mohammedraza Hassanali Mohamemdali kwa pongezi na ushauri alioutoa kwa wizara ikiwemo suala la kuwa waangalifu katika utoaji wa mikopo.

Mhe. Raza nakuhakikishia kwamba mikopo itazunguka Pemba na Unguja. Lakini nitahakikisha kwamba mikopo inarejeshwa. Huko nyuma watu walikuwa wanapewa pesa za mikopo wakawa wanasema aah! Pesa za JK na AK, si pesa za Marais wetu hizi tumepewa tu zitusaidie. Kwa hivyo, mara hii hizi ni pesa za wananchi wenyewe, anatakiwa mwananchi apewe atumie, akisha arejeshe ili na mwananchi mwengine na yeye apate.

Aidha, napenda kumjulisha kwamba wizara tayari imeunda kamati katika ngazi mbali mbali kwa ajili ya kusimamia masuala ya udhalilishaji wa kijinsia. Namuomba Mhe. Mohammedraza na Waheshimiwa wengine kuunga mkono kamati hizo katika maeneo yao. Wala wasisubiri njoo, kila mara muwe munaulizia jamani hatuna vikao vyovyote hapa, ndio viongozi tunavyotakiwa, maana uongozi usiitwe wewe lakini wewe mwenyewe ujipeleke.

Kuhusu suala la ajira napenda kumjuilisha kwamba liko chini ya Wizara ya Nchi (OR) Kazi na Utumishi wa Umma. Hatuna uwezo wowote wa kuajiri.

Mhe. Naibu Spika, namshukuru Mhe. Mwanaidi kwa pongezi alizozitoa kwa wizara. Hii inatokana na kwamba anafuatilia kwa karibu utendaji wa wizara hii na anatambua juhudi zetu tunazozichukua. Wengine wanasema tunatizama chini ya meza tu na viti, lakini Mhe. Mwanaidi anajua kwamba sisi tunafanya kazi. Masuala yake aliyouliza kuhusu fidia na jengo la ofisi ya idara ya ushirika tayari nimeshayatolea maelezo.

Mhe. Naibu Spika, napenda kumshukuru Mhe. Mahmoud Thabit Kombo kwa pongezi alizotupa. Aidha, nataka nitamke kwamba Mhe. Mahmoud Thabit Kombo ni mmoja wa Wajumbe wa Kamati ya Rais ya kusimamia uchangishaji fedha kwa Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi. Ni matumaini yangu ataendelea kushirikiana nasi kwa hili na mengine yote. Ahsante sana Mhe. Mahmoud Thabit Kombo.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa ametaka apatiwe ufafanuzi wa vifungu mbali mbali. Ufafanuzi wa vifungu hivyo ni kama ifuatavyo.

Kifungu 0301 Ofisi Kuu Pemba. Fungu la mishahara na maposho maalum limeongezeka kutokana na kuongezeka kwa idara tatu katika muundo mpya wa wizara pamoja na ongezeko la viwango vya mishahara na maposho kwa wafanyakazi.

Fungu la posho la vikao na Kamati. Fedha hizi ni pamoja na posho kwa ajili ya vikao vya kamati ya kupitisha mikopo, ukaguzi wa mahesabu, kufanya mapitio sheria ndogo ndogo za ushirika na ukaguzi wa vyama vya ushirika pamoja na posho la chakula kwa watendaji wanaokwenda kufanya shughuli za ufuatiliaji mikopo.

Fungu la viburudishaji na fungu la maendeleo ya wanawake. Tayari nimeshalitolea ufafanuzi katika majibu niliyoyatoa kwa Mhe. Ismail Jussa.

Fungu la huduma za studio. Gharama hizi ni kwa ajili ya kulipia muda wa kurusha matangazo kupitia redio na televisheni yanayohusiana na masuala ya uwezeshaji wananchi kiuchumi. Mwaka jana kifungu hicho hakikutengewa fedha, lakini mwaka huu imeonekana haja ya kutoa elimu juu ya masuala hayo kupitia vyombo vya habari.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu ufafanuzi wa jadweli na mchanganuo wa kesi kwenye ukurasa wa 79 namuomba Mhe. Mahmoud Muhammed atupe muda tulifuatilie katika wilaya na baadae tumtumie kwa maandishi.

Kuhusu suala la fidia tayari nimeshalielezea kwamba kifungu hiki tunacho na tunaishukuru Wizara ya Fedha imetupatia shilingi milioni 100, kwa ajili ya kuwalipa watu waliopatwa na matatizo kazini.

Aidha, kuhusu suala la ajira kwa vijana, ni kama nilivyoeleza katika programu za kuwawezesha wananchi, pamoja na miradi ya maendeleo, ambapo kuna programu za ajira kwa vijana.

Mhe. Naibu Spika, naomba sasa ambapo kuna *program* za ajira kwa vijana.

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea na majumuisho, sasa naomba nimjibu Mhe. Shadya Mohammed Suleiman, kwamba idadi ya malalamiko ya wanawake yaliyoripotiwa wizarani kwa mwaka huu ni 119 na kwa upande wa Unguja ni 24 na Pemba 95. Kati hayo malalamiko matano yalihusu kutelekezwa na waume zao. Aidha, ninamuahidi kwamba tutaendelea kutoa elimu kwa wanawake kwa ajili ya kuwaelimisha juu ya hatua za kuchukua iwapo wakikumbana na kadhia hii.

Mhe. Naibu Spika, siku hizi wanaume wanasema wanapigwa na wanawake, lakini hawaripoti kwetu, sasa hawa wanawake wanaripoti. Kwa hiyo, tutalifanyiakazi. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, kuhusu suala la ujenzi wa ukuta wa Welezo haikuwezekana kwa mwaka huu wa fedha. Hata hivyo, suala hili litafanyiwa kazi kwa mwaka 2015/2016.

Mhe. Naibu Spika, tunamshukuru Mhe. Asha Abdu Haji kwa ushauri wake na tutaufanyia kazi. Taaluma ya Ujasiriamali itaimairishwa ikiwemo katika maeneo aliyoyataja.Vile vile, wizara imekuwa ikitekeleza mikakati tofauti ya kuwaendeleza wanawake ikiwemo mafunzo ya ujasiriamali, kuviunganisha vikundi vya wanawake na huduma za mikopo, biashara, huduma nyengine za kitaalamu pamoja na Sera ya Maendeleo ya Wanawake ambayo imeainisha kwa kina namna ya kuwaendeleza wanawake. Kutokana na hali hiyo, naomba mashirikiano yake kwani hivi sasa tumo kwenye mambo ya mikopo, basi vyema afuatilie vikundi vyake, ili na wao wapate mikopo.

Mhe. Naibu Spika, wizara hivi sasa inao Mfuko mmoja wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi, ambao umejumuisha mifuko yote ambayo iliyokuwepo kabla, yaani utaratibu wa mikopo umeelezwa katika muongozo wa uendeshaji wa mfuko huo.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto, bado dakika 10.

Mhe. Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Naibu Spika, pia, nataka nimjuilishe Mhe. Mjumbe, kuwa fedha za Zakka zinasimamiwa na Kamisheni ya *Wakfu* na Mali ya Amana. Kwa kweli wizara ninayoisimamia mimi tangu nimeanza na wala sisemi uongo kwa sababu sijawahi hata mara moja kupokea fedha hizi na ziliishia na mwenzangu Mhe. Haroun Ali Suleiman. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, wizara ilipata fedha hizi mara moja tu na kuzigawa kwa watu wanaoishi katika mazingira magumu na kwa vikundi vya ujasiriamali wadogo wadogo kwa wilaya zote za Unguja na Pemba.

Mhe. Naibu Spika, sasa naomba nimjibu Mhe. Salma Mussa Bilali kwamba taratibu tunazotumia katika kuwafuatilia wateja wa mikopo kwa kushirikiana na masheha wa maeneo yao. Kutokana na utaratibu huo, basi baadhi ya wateja wameanza kulipa madeni yao na juhudi za ufuatiliaji zinaendelea na maswali yake mengine tayari nimeshayajibu wakati nilipokuwa nikitoa maelezo ya Waheshimiwa Wajumbe wengine. Hata hivyo, napenda kumshukuru tena Mhe. Mjumbe kwa pongezi zake alizotoa kwa wizara kwa kulipatia jengo la Afisi ya Idara ya Ushirika.Napenda kumuahidi kwamba wizara kwa mwaka huu litashughulikiwa.

Mhe. Naibu Spika, vile vile, kuhusu suala la kutokomeza vitendo vya udhalilishaji (vitangi), suala hili linashughulikiwa kwa kufanyiwa juhudi mbali mbali kama vile kutoa elimu kwa jamii, kuanzisha Kamati katika shehia za kupinga vitendo vya udhalilishaji, kupita skuli na kutoa elimu ya kujikinga na udhalilishaji kwa wanafunzi, lakini bado jamaa wametushika na wanawadhalilisha watoto na kuwabaka.

Mhe. Naibu Spika, pia, napenda kumshukuru Mhe. Fatma Mbarouk Said kwa pongezi zake alizozitoa kwa wizara. Pia, kuhusu masuala ya vifungu, kwa kweli vifungu hivyo tayari nimeshavitolea maelezo wakati nilipokuwa nikijibu masuala ya Wajumbe mbali mbali. Aidha, kifungu cha Likizo ni kwa ajili ya wafanyakazi 25 watakaokwenda likizo kwa kila mmoja kulipwa shilingi 100,000/=, yaani hawezi mtu kwenda likizo bila ya kulipwa shilingi 100,000/=.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Asha Bakari Makame, naye pia napenda nimshukuru kwa pongezi na michango yake kwa wizara na serikali na huyu ni Makamu Mwenyekiti wa Taifa kwa Upande wa Zanzibar. Kuhusu suala la Mfuko wa Zakka tayari nimeshalitolea maelezo wakati nilipojibu maswali ya Waheshimiwa Wajumbe. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, sasa napenda nimjibu Mhe. Ali Salum Haji kwa vituo vya kutoa wajasiriamali, basi tutachukua vijana wanaotoka Vyuo Vikuu vya Ufundi na wanaomaliza masomo ya Sekondari pamoja na wengine ambao watakaoamua kujiajiri kupitia ujasiriamali. Katika kituo hicho vijana hao wanaunganishwa na huduma za kifedha pamoja na huduma nyengine za ushauri kwa kujiendeleza na biashara zao.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu suala la uzio na fidia. Kuhusu suala la fidia tayari nimeshalitolea maelezo.Vile vile, kuhusu fungu la ununuzi wa gari Pemba, gari hii ni kwa ajili ya ufuatiliaji wa shughuli za mikopo Pemba ambapo kwa sasa shughuli hizi zinakwaza kutokana na kukosekana huduma hizi. Vifungu vya safari na huduma za wanawake na watoto tayari nimeshavitolea ufafanuzi.

Mhe. Naibu Spika, Fungu la Maendeleo ya Vijana zilizotengwa ndizo ambazo zinazohitajika kwa mwaka huu kwa ajili ya shughuli za Baraza la Vijana. Aidha, napenda nichukue fursa hii kuwaeleza Waheshimiwa Wajumbe kwamba kutokana na safari zinazofanywa watendaji wanapata fursa za kukutana na washirika wa maendeleo ambapo wanatusaidia katika miradi mbali mbali pia Tanzania imeridhia mikataba tofauti ambayo tunatakiwa kuitolea taarifa katika mikutano.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu Baraza la Vijana, naomba niseme kwamba Baraza hili tayari tumeshalifanyiakazi, sheria tumeshaitunga na ikaja hapa na kupitishwa na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na hivi sasa tumezipeleka kunakohusika, ili tukirejeshewa tu, basi tayari tunaunda Baraza la Vijana.

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea na majumuisho, namshukuru sana Mhe. Viwe Khamis Abdalla kwa pongezi zake na kuhusu Baraza la Vijana tayari nimeshalitolea maelezo. Hivi sasa wizara imo katika hatua za kutayarisha Kanuni za Baraza la Vijana, aidha, sheria hiyo ikeshakutiwa saini mchakato wa uanzishaji wa Baraza hilo utaanza rasmi na sisi tunataka kama leo liwe tayari. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, uwezeshaji unalenga pia kuwasaidia vijana na kuwakwamua kiuchumi, ili waweze kujiajiri. Kwa hivyo, ninawaomba Waheshimiwa Wajumbe, kuwahamasisha vijana katika maeneo yao kuutumia kikamilifu mfuko huu. Aidha, Kituo cha Mkono kwa Mkono tayari kimeshafunguliwa Micheweni Hospitali mwezi Disemba, 2013. Naomba radhi kwa maelezo yangu si sahihi, ni kwamba Kituo cha Mkono kwa Mkono tayari tumekifungua Wete na Micheweni bado. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Mussa Ali Hassan naye napenda kumjibu kwamba wizara kwa mwaka wa fedha imetenga jumla ya shilingi milioni 500,000,000/= kwa ajili ya utoaji wa mikopo kwa makundi mbali mbali wakiwemo vijana, wanawake na kadhalika.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu suala la Nyumba za Wazee wizara kwa sasa haina uwezo wa kujenga kwenye maeneo mengine. Kwa hivyo, naomba kwamba wazee ambao wako vijijini ni wazee wetu, basi tukae nao katika nyumba zetu kwa ajili ya kuwalea na kuwasaidia pamoja na kuwashirikisha katika mambo mbali mbali, kwani na wao walituzaa sisi wakatulea na kutuengaenga mpaka tukafika tulipofika na wala tusiisubiri serikali tutaingia dhambini.

Mhe. Naibu Spika, masuala mengine ya Mhe. Mjumbe tayari nimeshayatolea maelezo wakati nilipokuwa nikijibu hoja za Waheshimiwa wengine.

Mhe. Naibu Spika, naomba nimalizie kwa ndugu yangu au mwanangu pia ni mpenzi wangu wa siku nyingi katika Kikao hichi cha Baraza, maana tuko pamoja zamani mimi na yeye na sijui vipindi vingapi hivi sasa. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, kwa kweli namshukuru sana Mhe. Hamza Hassan Juma kwa michango yake yote aliyoitoa na yale aliyoyasema tumeyazingatia na tutayafanyiakazi tena mikopo atapata kwa watu wake na wala asiwe na wasi wasi. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, Aidha, napenda nimhakikishie pamoja na Baraza lako tukufu kwamba Mfuko wa Uwezeshaji utasaidia wananchi wote watakaotimiza masharti yote ya mikopo kwa Unguja na Pemba ikiwemo wananchi wa Mboriborini watapata mikopo. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, nawaomba wenzangu ambapo pengine nimesahau kuwajibu kwanza wanisamehe sana, lakini ninavyojua kwamba nimejitahidi sana. Naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Fedha: Mhe. Naibu Spika, naafiki.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, sasa niwahoji wale walioikubali Hotuba ya Wizara ya Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto kuhusu Makadirio ya Mapato ya Matumizi kwa mwaka wa 2014/2015, wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda. *(Makofi)*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa Baraza limejadili na kuikubali Hotuba ya Bajeti ya Wizara. Sasa naomba Baraza lako tukufu likae kama Kamati ya Matumizi kwa ajili ya kuvipitisha vifungu vya matumizi kwa Wizara ya Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto.

KAMATI YA MATUMIZI

FUNGU 28 - WIZARA YA UWEZESHAJI, USTAWI WA JAMII, VIJANA, WANAWAKE NA WATOTO

Kifungu 1001	-	Idara ya Ushirika	10,000,000/=
Jumla ya Fungu			**10,000,000/=**

Kifungu 0301

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, nitakuwa sitendi haki kama sikumshukuru Mhe. Waziri, kwa maelezo yake aliyotupa, lakini niseme rasmi kwamba hayaridhishi na yamekuwa ni yayo kwa yayo maji ya futi kwa nyayo. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kwa miaka mingi na Mhe. Waziri, mwenyewe ni shahidi, mimi nilikuwa sisimami katika bajeti ya wizara hii na hata nilipokuwa nikichangia katika vifungu nilikuwa sisimami, lakini nimeamua mara hii kusimama na kuhoji kwa sababu naona kama ninavyosema mara nyingi kwamba sehemu kubwa ya bajeti ya wizara hii ukitizama ni kuhudumia Afisi kwenda na kurudi, lakini tija hasa katika nchi haionekani.

Mhe. Mwenyekiti, sasa hapa hatuchangii tena hapa, isipokuwa mimi nataka bado Mhe. Waziri, anitosheleze na naanza hapa, lakini nitazungumza kwa kila Idara, kwamba tumeambiwa malengo ya serikali kwa mwaka huu ni kupunguza safari, warsha na semina na mambo kama hayo, lakini nikiitizama bajeti yake kuanzia Afisi Kuu Pemba mpaka mwisho kipaumbele chao ni safari na viburudishaji kwenye semina na mikutano, basi hakuna jengine. Kwa hivyo, naomba nianze kwa kunieleza kwamba kwa sababu hiyo, kwa nini tupitishe bajeti hii ikiwa tunaambiwa lengo la serikali kwenye bajeti ya mwaka huu ni kupunguza safari, kwamba Fungu la Safari katika Afisi Kuu Pemba limeongezeka kutoka shilingi milioni 15,000,000/= mwaka jana hadi milioni 25,000,000/= mwaka huu.

Mhe. Mwenyekiti, maelezo ya Mhe. Waziri, ametuambia kwamba safari zimeongezeka na watendaji wameongezeka, lakini nataka kusaidiwa na serikali kwa jumla kwamba hivi katika wizara tofauti, kuna mipango tofauti ya kufanya shughuli zao, kwa sababu tukienda wizara nyengine tunaambiwa kwamba Pemba anayekuja katika masuala kama haya mara nyingi ni Afisa Mdhamini labda na Afisa wake mwengine mmoja anayehusika na masuala ya fedha na mambo mengine yanamaliza kule kule.

Mhe. Mwenyekiti, sasa kama hali ni hiyo hata akiongezewa Idara bado Afisi Kuu Pemba inasimamia wizara kwa ujumla wake, katika vikao vinavyokuja hapa Unguja, ndio viongeze kutoka shilingi milioni 15,000,000/= hadi shilingi milioni 25,000,000/=, naomba katika hilo anitosheleze. Vile vile, moja nimemkubalia nitanyamaza na haidhuru nitakuja kutoa hoja nyengine, kwamba haya mengine ametuambia kuwa mafuta na vilainisho vimeongezeka kwa sababu zimeongezeka gari badala ya kuongezewa Idara.

Mhe. Mwenyekiti, lakini kwenye vifaa na huduma za Afisi na hapa nataka nitoe mfano mmoja tu, kwa sababu ya muda anisaidie. Katika suala la ununuzi wa magazeti na majarida kifungu 220508 mwaka jana ilikuwa shilingi 600,000/= na mwaka huu ni shilingi milioni 1,470,000/= kwa Pemba tu, ndio nikaona kuna sababu ya kuuliza kwamba hivi ndivyo vipaumbele vya wizara. Utakapokwenda kwenye mafungu yanayotoa huduma hasa zinazohusika huyaoni. Kwa hiyo, namuomba Mhe. Waziri, anipe maelezo ya kuniridhisha kwamba kwa nini tupitishe mafungu haya ambayo yanakwenda kuhudumia Afisi na utendaji badala ya kushughulikia zaidi kutoa huduma zinazohusika katika wizara ambazo zimelengwa kwa wananchi, naomba anipe maelezo Mhe. Waziri.

Mhe. Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Mwenyekiti, nimemfahamu sana Mhe. Mjumbe, kwamba mwaka jana tumeweka shilingi milioni 15,000,000/= na mwaka huu ni shilingi milioni 25,000,000/=.

Mhe. Mwenyekiti, lakini naomba Mhe. Mjumbe, akumbuke kwamba mwaka jana tulikuwa na Wizara ya Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto na mara hii wizara imekuwa kubwa. Sasa jamani tunataka huyu Afisa Mdhamini kule Pemba tumtembeze kwa miguu afuatilie kazi badala ya kutumia gari akatia mafuta na kuweza kwenda sehemu mbali mbali kwa ajili ya kufanyakazi na akimaliza shughuli huwa anakuja na kuturipotia. Kutokana na hali hiyo, Mhe. Mjumbe, anasemaje kuhusiana na hili au tupunguze kiasi gani hivi sasa. *(Makofi)*

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, namsikitikia sana Mhe. Waziri na haya nawasikitikia Waheshimiwa Mawaziri wote kwa jumla, kwa sababu mara nyingi tumesema wawe waangalifu na watendaji wao. Kwa kweli mimi ninahakika tukizipitisha hizi Mhe. Waziri hata kuziona hizi hazioni.

Mhe. Mwenyekiti, lakini nianze na lile la safari ambalo nililizungumza mwanzo ametuambia wakati alipokuwa akinipa maelezo ambayo niliyadai katika fungu la safari, kwamba kwa Pemba limeongezeka fungu la safari kwa sababu wameongezewa Idara na hili nilikuwa nikimsikiliza kwa makini sana, ambapo linahusu safari baina ya Unguja na Pemba kwa ajili ya kuhudhuria vikao na alinitajia orodha ya vikao.

Mhe. Mwenyekiti, nimesema kwamba unapoangalia utaratibu wa safari za kikazi na za ndani ni kwamba wanaokuja mara nyingi ni Afisa Mdhamini labda na Mhasibu wake, sasa mambo mengine wanamalizia kule kule za Idara zote. Katika Wizara hii kuna lipi kubwa kwamba kuongezeka Idara ambako wana mafungu yao huko kwamba, kwa nini kuwe kunaongeza idadi ya watu wanaosafiri baina ya Unguja na Pemba hata cha kuongeza gharama kiasi hicho.

Mhe. Mwenyekiti, lakini la pili, katika fungu hili kuna safari za nje Pemba kafika fungu hilo hilo la safari kuna safari za nje ilikuwa milioni sita mwaka huu imefika milioni kumi hii si baina ya kuja Unguja na Pemba hii, ndio maana nauliza tena kwamba, lakini naliuliza hili pia katika muktadha ule aliotwambia Waziri wa Fedha kwamba kwa mwaka huu wa fedha, serikali imeamua kwa makusudi kutoa agizo kwamba safari zipunguzwe, sasa tunachokiona katika bajeti ya kila Wizara inayokuja, sasa hivi tunajadili hii, lakiini kila wizara fungu la safari limebakia pale pale au limeongezeka, sasa unapotwambia serikali imetoa agizo kwamba safari zipunguzwe, mbona matumizi hayaakisi maamuzi hayo hilo moja.

Mhe. Mwenyekiti, na la pili, katika vifaa, sijasema mimi waende kwa miguu Pemba, lakini nilichokuwa nasema kwamba nimetoa mfano mahsusi, labda ajibu Mhe. Zainab hivi kwa kuongeza Idara tatu ambazo mwanzo walikuwa nazo nyengine kwa Pemba inaongeza gharama ya magazeti kutoka laki sita hadi 1,400,000/=, yaani Idara tano alizoongezewa zitatumia pesa zaidi za magazeti katika 1,400,000/= ukitoa 600,000/= zinabakia laki 8,070,000/=,

hivyo Idara tano ulizoengezewa zinatumia 8,070,000/= kuliko wizara nzima kwa Pemba, ndio wa mwanzo wanatumia laki sita.

Mhe. Mwenyekiti, haya ndio yanayoonyesha matumizi mabaya na ninaposema mara nyingi wanatoa mafungu wanapewa Katibu Mkuu akesha anakwenda kuchomeka chomeka wanavyotaka wenyewe namna wanavyozitumia na wanavyozihaulisha kutoka kwengine wanajua wao wenyewe, tumechoka Wawakilishi hapa kufanywa mihuri na kuidhinisha matumizi ya fedha za walipa kodi masikini, wanakwenda Hospitali hawana dawa, elimu wachangie, lakini matumizi ndio haya. Naomba majibu ya kunikinahisha kutoka kwa Mhe. Waziri.

Mhe. Waziri Ustawishaji, Ustawi wa Jamii, Vijana Wanawake na Watoto: Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka niseme hivi, Mhe. Mwakilishi naomba nikwambie katika watu duniani waliokuwa waaminifu ni wanawake na mimi huwa kuna safari za nje tele naziacha kwa sababu ya kufikiria juu ya hawa wanawake waliopo hapa masikini za Mungu, mimi nikitumia mafungu makubwa makubwa kama yale wao nitawasaidia vipi? Mimi huwa naacha kabisa, lakini sasa kwa vyovyote tukisema Zanzibar ni Unguja na Pemba sasa huyu Bi Maua huyu Afisa Mdhamini wakati mwengine naye hutakiwa asafiri nae aende katika mbio za mwenge, wakati mwengine huyu huyu Bi Maua hutakiwa afasiri aende Ulaya na Marekani huyu huyu Bi Maua au uwakilishi huo wa upande mmoja tu, watu watoke hapa wende na safari zao wale kule wawe hawana uwakilishi wowote, halafu kule watu wanakwenda wanazungumza mambo yao huku, hatuna uwakilishi wa mtu wa Pemba kusema kwamba tuna tatizo hili na hili.

Mhe. Mwenyekiti, mimi naomba nieleweke isijekuwa nabagua Pemba na Unguja, lakini naomba uwakilishi tunaposafiri lazima upatikane Unguja, lazima upatikane Pemba na haya ni sehemu ya kazi zetu, sisi hii kusafiri ni sehemu ya kazi zetu sio kwenda kujikumbia mapesa tu, sasa kama unaona aa, pesa hizi tusizitumie twambie ngapi tuzitowe tuwape wananchi na ngapi tuendelee nazo sisi.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, ili nisisimame tena kwa sababu sipendi kuonekana kwamba labda nakazania moja moja tu, nichukue Afisi kuu Pemba yote kwa ujumla wake ili nimsaidia Mhe. Waziri, Pemba jumla ya bajeti yake yote Afisi Kuu Pemba ni milioni 710,086,000 ipo katika ukurasa wa 287 pale, kwenye huduma hasa zinazolenga wananchi ni milioni 25 uzitizame hizo katika fungu la ruzuku kuna milioni 19,463,000/= ndio hapo kuna mfuko wa kujitegemea, pana maendeleo ya jamii mradi wa mafunzo, maendeleo ya wanawake zote ziko hapo jumla 19, halafu uchanganye na misaada ya kijamii ambayo ina fungu moja tu, maendeleo ya wanawake na watoto 5,235,000/= kwa jumla yake unapata kama milioni 25.

Mhe. Mwenyekiti, katika 710,000,000/= za Afisi kuu Pemba inayokwenda hasa katika tija kwa wananchi ni 25 milioni, hivi wananchi wa Zanzibar ndivyo wanavyojiuliza, kwamba hatuwezi tukawa na serikali inayohudumiwa watu mishahara wanaokwenda kwenda kazini na kurudi tu, lakini tija maana yake madhumuni ya kuunda Wizara, Idara ni kumpa huduma mwananchi. Sasa hichi kinachokwenda kwa wananchi ni 25, sasa mimi simwambii mimi nataka yeye Waziri aniambiye katika 710,000,000/- watendaji wake aniambie hivyo yeye karidhika katika hizo 25 milioni, ndio ziende katika huduma 685 zitafunwe na utawala tu, yeye karidhika Mhe. Waziri hilo.

Mhe. Waziri Ustawishaji, Ustawi wa Jamii, Vijana Wanawake na Watoto: Mhe. Mwenyekiti, ikiwa yeye hajaridhika nitakuwa na mimi sijaridhika, lakini naomba nimuulize sasa tufanye nini hapa?

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu sina, nitatumia *theory* inaitwa *Arbitrary*, mimi ningesema fungu la safari kwa upande ule zingewachwa angalau zile za mwaka jana, lakini vile vile, katika haya mafungu mengine ya vifaa na huduma, naamini kama zingechukuliwa angalau milioni kumi kumi katika mafungu haya zikapelekwa hapa tungeona angalau zinakwenda kuimarisha huduma Pemba, lakini hili ni moja.

Mhe. Mwenyekiti, niseme kusema hivi, haina maana kwamba tumeisaidia sana na mimi nasikitika sana kwa sababu tunaweza kuyasema hayo baadae namna wanavyotumia, tunajua sote Kamati humu hupati maelezo ya kutosha watu wanahaulisha wanavyotaka wao ndani ya Wizara. Kwa hivyo, hata hiyo kusema zikatwe zipelekwe hapa, mimi nataka wao waje watwambie na Kamati husika wapo, lakini mimi ningelisema kwamba angalau katika mafungu hayo la safari, la gharama za mafuta na vilainisho, vifaa na huduma za Ofisi pangepunguzwa angalau milioni kumi kumi zikapelekwa hapa katika huduma kwenye ruzuku na kwenye misaada ya kijamii zikenda kuwasaidia wananchi wenyewe wahusika naomba hilo.

Mhe. Waziri Ustawishaji, Ustawi wa Jamii, Vijana Wanawake na Watoto: Mhe. Mwenyekiti, mimi naomba tu nimkumbushe Mhe. Jussa kwamba katika vifungu hivi kule Pemba kuna mambo ya mishahara tusije tukaona kwamba tuna pesa nyingi tulizozipanga sisi, tukaja tukawanyima watu haki zao na bajeti, mimi ninavyojua hii tumeipitisha kwenye Kamati yetu ya Ustawi wa Jamii Wanawake na Watoto na tukawaeleza yote na wakayakubali. Sasa kubadilishwa hapa na sisi tumepanga kwa mujibu wa mahitaji ya pesa hizi Je, Mhe. Jussa, unaona unatutendea haki Wizara hii ya Uwezeshaji Wanawake na Watoto.*(Makofi)*

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nadhani utaratibu, sio mimi kuulizwa masuala, mimi kazi yangu ni kumuuliza masuala waziri ajibu, ndio kazi yake hapa ndani, ikiwa yeye ananiuliza mimi masuala itabidi mimi anipishe mbele nikakae waziri wa Uwezeshaji, aja akae katika kiti changu hapa, la kama kazi haiwezi amuombe Mhe. Rais ataweza kumpumzisha na atafute mwengine anayefaa.

Mhe. Mwenyekiti, mimi ninachosema tena, mimi akinambia kwamba hivi ndivyo tulivyopanga, najua ndivyo alivyopanga, ndio maana tukaletewa buku hili, ninachohoji mimi kama mwakilishi natakiwa nipitishe matumizi haya kwa niaba ya walipa kodi wakiwemo Mji Mkongwe ni kwamba je, matumizi haya ndio kipaumbele chetu kwa nchi masikini, kila wakati tunalia umasikini tunatanga kiguu na njia kwenda kutafuta misaada na mikopo kwamba tukizipata haya, ndio matumizi yake tunawaambia wananchi wa Zanzibar, Serikali hii ndio inajielekeza huko, tunaambiwa kila siku hapa inatekeleza ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi tunaambiwa kila siku, ilani ya uchaguzi ndani ya Chama cha Mapinduzi kipaumbele chake ndio kwenda kutumia katika utawala maofisini badala ya kuhudumia wananchi katika mambo yao ya msingi, mimi siliamini hilo.

Mhe. Mwenyekiti, sasa ninachosema mimi ni kwamba yeye akisema kwamba aachiwe, mimi mwisho nitafanya maamuzi nitaondoa shilingi yangu, lakini ninachosema ni kwamba mimi nilikua nadhani kwamba hili tumepiga kelele tokea mwaka wa mwanzo wa serikali hii 2011, kwamba imefika pahala tutizame vipaumbele vyetu tumechoka kuhudumia mambo ya utawala maofisini, lakini inakuwa zile huduma zenyewe hakufiki kitu na ndio maana kila mwaka bajeti ni yayo kwa yayo, hakuna jipya, kwa sababu kila kitu alichozungumza Mhe. Waziri, hili tayari, sera tayari na sheria tayari, lakini ukienda kwa wananchi, hakuna chochote tunachokiona. Kwa hivyo, aseme kama yeye anaridhika kwamba aachiwe mimi langu moja tu, nitaondoa shilingi yangu, haki hiyo ninayo, lakini ninachosema mimi kwa niaba ya wananchi, nasema siridhiki na huku ni kuwadhulumu wananchi wa Zanzibar, badala ya kutumia kuwahuduma tunatumia kujinufaisha sisi maofisini kwetu. Ahsante sana.

Mhe. Mwenyekiti: Kwa hivyo, tuendelee.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, endelea

Kifungu 0301	Ofisi Kuu Pemba-	710,086,000/=

Kifungu 0401 Idara

Mhe. Ali Salum Haji: Mhe. Mwenyekiti, ahsante, nashukuru wakati nikichangia nilitaja fungu katika ukurasa 288 na fungu nililokuwa nikilichangia ni la gharama za safari fungu 220300 ambalo mwaka jana lilitengewa Shs. 47,960,000/= mwaka huu limekwenda zaidi ya nusu milioni 75,870,000/= na nikataka maelezo ya kutosha katika zile hoja ambazo na mimi zilinisikitisha na nikatolea mifano katika baadhi ya vifungu vya mbele ambavyo vimenyimwa fedha, lakini fedha zimekwenda kwenye safari na vifungu ambavyo vya mbele nimevizungumzia, vilikuwa vinahusiana na masuala ya kijamii Maendeleo ya Wanawake na Watoto pamoja na masuala ya vijana.

Mhe. Mwenyekiti, sasa ndio hapa nikataka maelezo ya kutosha sababu ya kuweka fungu kubwa kwenye safari hizi tukapunguza mafungu kwenye masuala ya maendele ya wanawake na watoto na maendeleo ya vijana nataka maelezo ya kutosha kwa Mhe. Waziri.

Mhe. Waziri Ustawishaji, Ustawi wa Jamii, Vijana Wanawake na Watoto: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli bajeti ya mwaka huu kwenye mambo ya safari imewekwa kubwa sikatai na huyu wanawake na watoto kusema kweli mara hii alikuwa nafaari nyingi na alipata shida sana kwa kushughulikia mambo haya haya ya wanawake na watoto, sasa ndio mara hii tukaona aibu ile isitokee tena, ndio hili fungu likafanywa liwe kubwa kuliko mwaka jana.

Mhe. Ali Salum Haji: Mhe. Mwenyekiti, majibu na mimi hayaniridhishi kabisa, kama Mhe. Waziri, anaona aibu watu kukosa safari akawaonea aibu wananchi wa nchi hii wakateseka vijana na wanawake, naomba bado anieleze sababu za msingi, hiyo safari ambazo wao wamezikosa zilikuwa zina manufaa gani zaidi kuliko manufaa ya wananchi wetu anambie tu au hizo safari zimeingiza nini katika hii kasma ambayo tumewawekeya kwa sababu tatizo ni *benefit. S*afari kila mtu anataka hata kama hujapata unajisikia aibu, lakini tunafaidika na nini wakati wananchi tunawawekea mafungu madogo wananchi ambao wana matatizo.

Mhe. Mwenyekiti, anijibu suala langu kama Mhe. Waziri, anaona bora aibu ya yeye kwenda safari za nje, lakini hajisikii aibu vijana na wanawake wa nchi hii kuteseka, naomba majibu yakutosha.

Mhe. Mwenyekiti: Kabla Mheshimiwa hajaendelea niliona na mimi nilivyofahamu mimi labda na wewe tuko sawa utasema, safari za nje sio za kwenda kutembea, sasa hivi tuko katika dunia tunajiunga katika mashirikisho mbali mbali, sasa ikikaribia muda mnapewa mwaliko mnakwenda kule si safari za kutembea, ni safari za kikazi ndio alivyokusudia, lakini nampa mwenyewe waziri aendelee kujibu.

Mhe. Waziri Ustawishaji, Ustawi wa Jamii, Vijana Wanawake na Watoto: Mhe. Mwenyekiti, na mimi nakushukuru kwa kunisaidia, lakini nataka niseme kuwa safari za nje haina maana kuwa ni kwenda kutembea tu, kwa sababu sisi tuna mikataba mbali mbali na umoja wa Kimataifa, halafu tunakokwenda kule tunapata misaada mbali mbali ambayo inakuja huku kusaidia wanawake na watoto. Sasa tukiambiwa kwamba tunajiwekea safari tu, sisi kwa manufaa yetu kwa kweli hapa sivyo hivyo tunavyokusudia.

Mhe. Ali Salum Haji: Mhe. Mwenyekiti, mimi naomba Mhe. Waziri, anisaidie moja tu ili kujiridhisha hizo safari nitajua kuwa ni safari gani na hiyo faida tuliyopata ilikuwa ni faida gani, labda kidogo naweza kujitosheleza.

Mhe. Waziri Ustawishaji, Ustawi wa Jamii, Vijana Wanawake na Watoto: Mhe. Mwenyekiti, hawa "*Save the Children"* wanatusaidia sana katika mambo ya wanawake na watoto na mimi nilieleza hapa kwenye kitabu changu kwenye ukurasa wa 64, watu wanaotusaidia wa Umoja wa Ulaya, nikasema India, Jamhuri ya Watu wa China, Mashirika ya Kimataifa, ikiwemo *UNPA, UNICEF, UNESCO, UNDP, ILO, Save the Children* na *FHI,* wote hawa wanatusaidia sisi na sisi tunakwenda kushiriki kwenye mikutano yao na tukiwa hapa wao wenyewe wanatoa mafungu ya pesa kuchangia katika Wizara yetu sisi ili kusaidia mambo ya wanawake na watoto, sasa kama atasema tusende huko, tukae tu hapa jamani yatakuwa haya.

Mhe. Ali Salum Haji: Mhe. Mwenyekiti, Taratibu kidogo, unajua Mhe. Waziri, anani-*quote* vibaya na anachonijibu sicho ambacho ninachotaka maelezo, tunajua tuna wafadhili wanatusadia, tunajua tuna ushirikiano wa nchi mbali mbali, lakini tunachokililia hapa ile safari ambazo wanazozitengeneza na mimi nilichomuuliza Mhe. Waziri, safari ambazo wamekwenda mwaka jana ambazo wao wakahisi pesa haikutosha, zilikuwa ni safari gani? Na nikataka kujua katika hizo safari tumenufaika na nini? Maana yake anieleze tumekwenda *UNESCO,* lakini tumekuja na mradi fulani ndicho nilichokuwa nakihitaji mimi.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri, anasemaje Mjumbe kwamba safari uliyokwenda mwaka jana zimezaa kitu gani hilo tu basi?

Mhe. Waziri Ustawishaji, Ustawi wa Jamii, Vijana Wanawake na Watoto: Mhe.Mwenyekiti, ahsante, kwanza nataka nikwambie Mhe. Ali Salum Haji ni Mjumbe wa Kamati ya Maendeleo na Ustawi wa Jamii na mimi nilikwenda mbele ya Kamati na akavikubali vifungu vyangu vyote, leo anakuja kuniuliza mwaka jana nimepata nini mimi, basi mwaka jana hatukwenda sie.

Mhe. Ali Salum Haji: Mhe. Mwenyekiti, kuna tatizo ndani ya Baraza la Wawakilishi na tatizo hili lipo kwa mabosi tunapozungumzia utaratibu wa vikao kwa mujibu wa utaratibu wa Kanuni tunakuwa tunapindishwa pindishwa tumetoka dakika 30, tumekuja dakika 20, leo asubuhi tumeanza kuchafuana hata katika Kamati utaratibu wa Kamati *at list* mtu apate siku mbili, unakwenda kwenye Kamati, Kamati yenyewe hata ukifika unafika saa 3 au saa 4 au tano saa nane hamna kitu, huwahi kuangalia kitu, tunafinywa ndio maana tunatafuta fursa nyengine za kuweza kuhoji. Sasa hebu tuwekeeni ule muda kwa mujibu wa taratibu za Kanuni ambayo tumeizungumza leo tumeandaa Kanuni, lakini mabosi wanapinga, leo hii tunaambiwa huenda kikao kikamaliza tarehe 24 asubuhi tumeanza kuchafuana. Mhe. Waziri, pamoja na kupapatua hakunijibu masuala sijaridhika, naomba nikae tuendelee.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, na mimi nataka niseme kwamba Mhe. Waziri, kanijibu kwa mpigo na zile hoja zangu hasa nilizouliza kwa kifupi hakunijibu, lakini mimi Mhe. Zainab kama alivyosema kanilea humu barazani.Kwa hivyo, nitafanya nae kazi chini ya Ofisi yake mwaka mzima huu ili kuhakikisha yale yote niliyoyasema anayatekeleza, lakini hili moja na nitaomba pia Mhe. Waziri wa Fedha, atusaidie, nimekuwa nikizungumza, sasa hivi kwa muda karibu miaka 3, baada ya kuona faida wa wenzetu Jamhuri ya Muungano kuanzisha benki ya maendeleo ya kinamama.

Mhe. Mwenyekiti, na mimi nilishauri mwaka uliopita na uliopita tena na mwaka jana nilikuwa na matumaini makubwa kwamba serikali imeshaanza kuwa katika hizo *processes* na niliomba serikali kupitia aidha Mfuko Mkuu wa Serikali kutengeneza mtaji wa kuanzisha hiyo benki na hivi leo nilipochangia. Pia, nilishauri kwa sababu sasa hivi ukiangalia wenzetu Bara kumeanzishwa ule utaratibu wa kuuza hisa na nikashauri, basi alau serikali kwa sababu Waziri wa Fedha mwaka jana alinambia kwamba uanzishwaji wa benki kwa sera za *BOT* lazima ianze na bilioni 15,000,000,000, ingawa mimi ile sikukubaliana nayo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu bilioni 15 inategemea na *population* wale watu ambao inohudumiwa na ile benki. Nikawaambia kwa upande wa Zanzibar sisi tuko milioni 1.3 Tanzania Bara wapo milioni 45,000,000. Kwa kule kuwa kuanzisha mtaji wa bilioni 15,000,000,000 sio tatizo, lakini alau kwa Zanzibar wazungumze na wenzao wa BOT ili alau kwa Zanzibar ianze alau bilioni 5,000,000,000 au bilioni 10,000,000,000, lakini hata hiyo ya bilioni 15,000,000,0000 nimejaribu kumshauri Mhe. Waziri kutokana na muda labda hakupata kutoa ufafanuzi, angalau serikali yetu ingelitwambia alau wataanzisha *Capital* ya bilioni 8,000,000,000, halafu bilioni 7,000,000,000 zilizobakia wauze hisa.

Mhe. Mwenyekiti, humu nilieleza kuna Wajumbe wanawake wameingia kwa nafasi za wanawake, naamini wengi wao wangelinunua hisa, sisi wenye majimbo ambao kuna wanawake tungelinunua hisa, kuna Wazanzibari wengi waliokuwepo nje wanauliza hakuna miradi ya kununua hisa Zanzibar. Wafanyabiashara na wananchi wangeliweza kununua hisa. Sasa kama tatizo la mtaji tumeshatoa ushauri, basi hebu serikali itwambie itusaidie na kwa kuwa hiyo benki atakayoanzisha mtaji atatoa Waziri wa Fedha, basi hebu amsaidie Mhe. Waziri, ni namna gani wanaweza wakatusaidia kuanzisha hii benki ya maendeleo ya akinamama kuondoa matatizo madogo madogo.

Mhe. Waziri wa Fedha: Mhe. Naibu Spika, nimemsikiliza vizuri sana Mhe. Hamza na hoja ya kutaka kuanzishwa benki ya kinamama au benki ya wanawake. Nimeeleza mwaka jana kuanzisha benki kunahitaji mtaji wa bilioni 15,000,000,000 na baada ya mazungumzo kati yetu, tumebaini kwamba tusianzishe benki ya wanawake kwa sababu bilioni 15,000,000,000 ni nyingi kuanzisha benki ya wanawake na hizi taratibu za kuanzisha benki ziko kwa Tanzania nzima, hazitegemeani na *population* kwamba Zanzibar *population* yake ndogo zile taratibu ziko *Uniform* ukianzisha Zanzibar, ukianzisha popote kule.

Mhe. Naibu Spika, lakini tumekubaliana na nataka nimuhakikishie Mhe. Hamza kwamba mchakato unaendelea na kama sio kila pahala unaposikia mchakato uwe unaanza kupiga mayowe wakati mchakato wenyewe haujakaa sawa. Tumekubaliana kwamba tutaanzisha kitu kinaitwa *Community Bank*, lakini itajumuisha wanawake, itajumuisha na ushirika, ili tuweze kuvipata vyama vya ushirika navyo viweze kuweka mtaji wao na kukuza ile *community*, lakini baadae benki hii au *Community Bank* hii itakuwa na malengo baadae kui-*turn* iwe ni benki kamili ya kibiashara.

Mhe. Naibu Spika, tumetoa mfano kama Dar-es-salaam *Community Bank* imeanzishwa hivyo hivyo *Community Bank, Dar-es-salaam Community Bank*, lakini sasa hivi wamekuwa wanaweza wakui-*turn* ikawa ni benki kamili na kuanzisha *Community Bank* sasa hivi unahitajia 2.5 billion. Tumefanya tumeziangalia *Saccoss* zote na mitaji waliyonayo ndani ya *Saccoss* na nadhani sasa hivi tunakamilisha zile taratibu za kibenki tuweze kuona kwamba benki hii itaanza na makao makuu yake yatakuwa wapi kwa upande wa majengo na watumishi gani tunaweza tukaanza kwa kuwaazima, lazima ianze kwa kuazima.

Mhe. Naibu Spika, lakini vile vile, nataka niseme kwamba hata hiyo benki ya wanawake haikuanzishwa kwa muda wa mwaka mmoja. Mimi ninajua taratibu zake zimechukua zaidi ya miaka 4 mpaka imekua pale ilipo na sisi tunakwenda na waziri anaweza akatoa tangazo kwa wale wote ambao wanaotaka kununua *share* katika ile *Community Bank* wakaanza kujiorodhesha na kuanza kulipia baadae itakapokuwa benki kamili watakuwa wana mtaji wa kutosha.

Mhe. Naibu Spika, lakini vile vile, tulieleza kwamba serikali hatutoweza kuingia sasa hivi ndani ya benki hii, kwa sababu moja kubwa *PBZ*, ndio benki ya serikali pekee hivi sasa inahitajia *Capitalization* kubwa sana *PBZ.* Inahitaji kuongezwa mtaji na serikali, sasa hivi iko katika harakati za kuitafutia mtaji kuiongeza *PBZ*, hii tungelipenda ianze na kuwa ni *Community Bank.* Tunaweza tukaanza kuichangia ile ya wanawake ilianza kwa kutoa michango hata benki yenyewe bado na watu wakatoa michango yao na mimi mmoja nimetoa mchango wangu ndani ya benki ile ya wanawake, lakini mwaka jana ndio nimepewa *certificate* yangu, mchango wangu niliutoa, nadhani ilikuwa ni mwaka 2008 au 2007. Kwa hivyo, michango inaweza ikaanza kukusanywa *certificates* zikaja baadae.

Mhe. Naibu Spika, kwa hivyo, nataka nimwambie tu Mhe. Hamza kwamba hatuko kimya kazi tunaifanya tunakwenda, lakini tumeona kwamba kuwaweka wanawake peke yao kwa mtaji ambao tunaoutaka tutachelewa. Kwa hivyo, tumeviingiza na Vyama vya Ushirika na *Saccoss*. Kwa hivyo, orodha ya vyama vyote na *account* zao na viwango vyao vya pesa na *contribution* yao tunaiandaa na tutakapokuwa tayari, mimi nadhani katika kipindi kifupi kijacho hiyo benki itaanza, lakini tutaianza huko na nasema ni vizuri kuanza huko kwa sababu hata mkiharibikiwa, mnaharibikiwa katika mtaji mdogo, mnaweza mkajirekebisha, kuliko mkaanza kuharibikiwa kwenye mtaji mkubwa wa bilioni 15,000,000,000, kujirekebisha nako kutakuwa kuna gharama kubwa.

Mhe. Naibu Spika, kwa hivyo, mimi naomba tu Mhe. Hamza na Waheshimiwa wengine walioiuliza kuhusu habari ya benki ya wanawake wavute subira, lakini katika hatua ambazo tunakwenda nazo na nadhani kwamba ni hatua nzuri sasa hivi tulipo.

Mhe. Naibu Spika: Tunarudi Barazani kwanza kwa sababu muda unakaribia kwisha.

(Baraza lilirudia)

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, kwa kuwa kazi yetu haijesha na muda unakaribia kuisha, namuomba Mhe. Waziri wa Fedha, atoe hoja tuongeze muda.

Utaratibu

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Naibu Spika, kwa kutumia Kanuni hii hii ya kuongeza muda, naomba nitumie fursa hii kukutaka wewe Mhe. Naibu Spika, usimtake Waziri wa Fedha kutoa taarifa ya kuongeza muda katika Baraza hii kwa sababu kwa mujibu wa programu tuliyopewa tulipokuja tuliambiwa Baraza hili litamalizika siku ya tarehe 30 Juni 2014. Sasa tuko mbele karibu siku tano ya ratiba tuliyopewa mwanzo na kwa kuwa leo itakapofika saa 8.00 tunakwenda mazikoni kwa mwenzetu hapa kwa sababu amefiliwa na mama yake Mhe. Zahra na kwa kuwa tuko mbele ya *program* kwa muda wa siku tano, naomba Baraza hili liahirishwe hivi sasa na hii bajeti ya Mheshimiwa mama yetu pale tuje tuipitishe kesho tukijaaliwa *biidhinillahi* kwa sababu muda upo wa kutosha, kwa sababu tuko mbele sana ya *program*. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa. ninakushukuru. lakini habari ya kifo waliokwenda mazikoni wameshaniaga na ruhusa nimewapa waliobakia tunaendelea na kazi. Kwa hivyo, Mheshimiwa atengue Kanuni tuongeze muda tumalize kazi.

Mhe. Waziri wa Fedha: Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa shughuli tulizojipangia bado zinaendelea na kwa kuwa muda umekaribia kufika, naomba tutengue Kanuni ili tuendelee na shughuli ambayo tumejipangia inayoendelea hivi sasa hadi tutakapomaliza.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa, niwahoji wale wanaokubaliana na hoja aliyotoa Mhe. Waziri, wanyooshe mikono.

Waheshimiwa Wajumbe, naomba kuahirisha kikao hadi saa 11.00 za jioni.

(Saa 12.55 Baraza liliahirishwa hadi saa 11.00 jioni)

(*Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia*)

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Naibu Spika, naomba radhi kwa kusimama ghafla, lakini nadhani kwa hatua iliyopo sasa hivi ya Kamati ya Matumizi ni hatua ya maamuzi na idadi ambayo tumo humu ndani haitoshelezi kuweza kufanya maamuzi. Kwa hivyo, nilikuwa naomba tupate muongozo wako kuhusu hili. Ahsante.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, tunaahirisha kikao kwa dakika tano Wanadhimu wahimize Wajumbe wao kuingia kwenye kikao.

(Saa 11:05 jioni Baraza liliahirishwa hadi saa 11:10 jioni)

(Saa 11:10 jioni Baraza lilirudia)

KAMATI YA MATUMIZI

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, imebidi kusimama tena kwa suala lile ambalo nilisimamia mapema kama Kanuni zetu zinavyoongoza Kanuni ya 72 (2) inasema au labda nianze 72 (1) inasema;

> "kiwango cha vikao vyote vya Baraza vitakuwa ni nusu ya Wajumbe wote".

Na 72 (2) inasema;

> "Mara kabla ya uamuzi wowote kufanyika ikiwa Mjumbe yeyote atakayehudhuria atapinga kwa kudai kwamba mbali na Mhe. Spika, Wajumbe waliopo ni chini ya nusu ya Wajumbe wote, basi kama Mhe. Spika atathibitisha kuwa Wajumbe waliopo ni chini ya nusu ya Wajumbe wote atasimamisha shughuli kwa muda wa dakika tano na huku muhudumu kwa maelekezo ya Katibu akipiga kengele kwa vituo, yaani siyo mfululizo".

Mhe. Mwenyekiti, tatu, endapo Mhe. Spika amesimamisha shughuli kwa mujibu wa fasili ya pili ya Kanuni hii, basi wakati wa Baraza akarudia shughuli baada ya wakati uliotajwa kisha atahakikisha kama idadi ya Wajumbe waliyopo bado imepungua nusu ya Wajumbe wote na kama itakuwa ni hivyo, basi ataliahirisha Baraza mpaka kikao kingine kinachofuata.

Mhe. Mwenyekiti, sasa nimeamua kusimama kwa sababu kama ninavyosema shughuli tunaifanya sasa hasa ya kupitisha vifungu kwa msingi wake ni shughuli ya maamuzi, kwa sababu ni shughuli ambayo inapitisha matumizi, ndiyo maana niliomba muongozo wako kwa sababu Wajumbe waliomo ndani humu bado tulikuwa kama 25 sijui labda kaongezeka kama mmoja…

Mhe. Mwenyekiti: Sasa hivi tuko 30 kwa sababu watu ndiyo wamekwenda mazikoni jioni wengine ndiyo wanakuja, tuko 30 sasa hivi.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, sasa Wajumbe wanaohitajika tufanye maamuzi ni angalau Wajumbe 41 kwa sababu jumla ya Wajumbe ni 81. Kwa hiyo, zaidi ya nusu au angalau nusu, basi ni 41. Nilikuwa naomba kulizingatia hilo, kwa sababu hiki ni chombo kikubwa ni muhimu kuzingatia taratibu tulizojiwekea katika kufanya maamuzi. Ahsante sana.

(Baraza lilirudia)

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa, kutokana na Kanuni kwamba mpaka hivi sasa tushaahirisha mara ya kwanza na sasa hivi mara ya pili haijatimia, naahirisha kikao hiki hadi kesho tarehe 11 siku ya Jumatano saa 3:00 asubuhi.

(Saa 11:16 Baraza liliahirishwa mpaka tarehe 11/06/2014 saa 3:00 asubuhi)